# MWONGOZO WA KANUNI ZA MATENGENEZO KUHUSU MAVAZI



Roho ya Unabii ikishirikiana na Enendeni Mitandaoni Kote

JE, NAPOVAA nguo nasema Moyoni, wacha nivae leo kwa Utukufu wa MUNGU?

Je, napoweka rangi kwenye makucha, napochana nywele zangu au kusuka au kuweka chale au kupaka rangi mdomoni, au kuvaa tai au pambo lolote, naona kwamba nafanya vile kwa utukufu wa Mungu? Sketi zilizobana kiuno za hoops ambazo gagulo lake lilikuwa la waya au mifupa ya samaki na kuchanua kama mwavuli zilikuwa ndiyo mtindo wa siku zile za miaka 1800. Kuharibika kwa afya hakumletei Mungu Utukufu. Kuvaa ni fasheni na pia utamaduni, mfano mwanamke wa Kihindi anapovaa sari, huwa anacha tumbo nje! Je, sisi tuvae kwa utamaduni wetu au kwa fasheni au kwa kumtukuza Mungu? Hakika kumtukuza Mungu iwe kipaumbele, na kisha utamaduni na fasheni namba mbili. Kwani fasheni na tamaduni nyingi zina mavazi mazuri tu, ambayo unaweza kuyafanya yaweze kumtukuza Mungu bila ya kukugharimu chochote zaidi. Nguo zangu zikoje? Je, ninavika yatima, wajane na masikini, kabla ya kujirundikia nguo nisizozihitaji, au ambazo sio za lazima?




SHUKRANI KWA MWENYEZI MUNGU

WA MBINGUNI

## *TABARUKU*

**Shukrani kwa Baba wa Mbinguni na Watafsiri, Waombezi, Wahariri, Washauri, Wataalamu wa Teknolojia, na watia moyo wote**

1. **Grace Momadi-Masaka-Jersey, Marekani**
2. **Gibson Wilson Mujuni- Bukoba, Tanzania**
4. **Ellen Sarah Nyagori- Rorya, Tanzania**
5. **Cindy Tustch- Washington State, Marekani**
6. **David Masaka -Pennslyvania, Marekani**
7. **John Mugane-Boston, Massachusets**
8. **Judi Mmari-Mugane-Kilimanjaro, Tanzania**
9. **Musa Budodi-Kahama Tanzania**
10. **Mbusi Mpagalushu- Bariadi, Tanzania**
11. **Daniel Nyangaresi Masaka- Kisii, Kenya**
12. **Paul Denis Masaka-Oklahoma, Marekani**
13. **Baraka Ndege Aruya-Morogoro, Tanzania**
14. Ghati Mambiso-Tarime, Tanzania

FIKIRIA HAYA KABLA HATA YA KUFIKIRIA HELENI NA MIKUFU: Riboni au lesi zilizopitiliza kichwani au kwenye mavazi, saa mikononi zinazomeremeta kuzidi hata bangili. Vipini kwenye nguo (brooch) vinavyomeremeta na kuvuta macho ya watu kuzidi hata mikufu. Maridadi kwenye nguo na kwenye nywele kama vile shanga nk au hata nguo za gharama mno kama vile suti ya dola 5000,nguo za wanawake za mamia ya dola, utailinganishaje na heleni za dola moja? Na Je, unaonaje kuhusu rangi za kucha na midomo zinazovuta macho ya mtu kuzidi hata tatoo au chanjo za ngozi?




# DIBAJI

SISI NI MABALOZI na MAWAKILI wa MUNGU- Je, Kwanini Tunavaa Nguo? Je, ni vibaya wanawake kuvaa suruali? Je, Mavazi ya heshima ni Yapi? Kwanini Wakristo wana mavazi ya kukosa adabu kuliko Waislamu?
Jipatie kitabu cha Mavazi kwa muumini, bure, soft copy

## Je, MWANAMKE AVAE SURUALI?

**Kuhusiana na Mavazi ya zamani ya watu wa Biblia, wanaume na wanawake walivaa majoho, na ndani waliweka suruali au kaptura ndefu. Mavazi ya Haruni ni mfano unaopaswa kujifunzwa, maana kuna kile MUNGU alimwambia avae kwa kujistahi na kumheshimu Mungu hata katika miaka ya 1800. Vazi lililopendekezwa lilikuwa na suraali ndani na kufanana na vazi la wahindi liitwalo Punjabi. Kwa vile leo suruali ni vazi la mwanamume ni vyema mwanamke asivae vazi hili kutokana na utamaduni wa dunia hii. Hata hivyo kuvaa suruali yenyewe bila ya blausi isiyobana inayofika chini na kufunika matako kutokana na maumbile ya mwanamke inamfanya mwanamke ajionyeshe kuwa hajavaa kwa kujisitiri au heshima. Hivyo kwa mwanamke anayevaa suruali ni vyema ajue jinsi yakuvaa blauzi refu kama ya aina ya Panjabi**

wanavyovaa wahindi au ile ambayo isiyobana na inafunika matako.
Sasa mambo haya ni endelevu kadri tunavyomjua Mungu na jinsi mitindo inavyoingia, hatupaswi kuparamia kila kitu na kuwa wa kwanza katika mambo ya fasheni. Watoto wasichana wadogo pia wafundishwe haya wakiwa wadogo, jinsi wanavyopaswa kuketi hata wakiwa kwenye mimbari nk, wasikae katika mimbari wakati wakihudumu au wakisimuliwa visa vya Biblia huku nguo za ndani zinaonekana, au wanajaribu kuvuta-vuta nguo ili zifike magotini. Nguo inapaswa kufika angalau chini kidogo ya magoti, wakati mtu amesimama au amekaa.Watoto pia nao wanapaswa kuvalishwa kaptura ndani ya magauni yao kwa vile wanacheza na kama watoto hawawezi kuangalia mambo mengine. Naweza kusema hata kwa watu wazima wengi kuvaa kaptura au suruali ndani ya gauni husaidia katika kuinama na kufanya kazi fulani, endapo gauni halimsitiri mtu vizuri, Kuhusu nguo za kuogelea watu wengi wana nguo za kuogelea za heshima, nimekutana na wasichana wa Kiarabu wanaogelea na wamevaa mavazi ya adabu tu, hatuna haja ya kuigiza utamaduni wa magharibi, hakuna haja ya kujionyesha kwa wengine kwa kuvaa vichupi vidogo na visidiria.
Ila napenda kusema kwamba kuvaa suruali yaweza kuwa jambo la lazima kwenye sehemu za baridi. Yaani Wakati wa Baridi kali. Mfano kwetu wakati wa baridi

ni -26 Centigrade. Hii ni baridi kali, wakati kama huu ninavaa suruali mbili au hata tatu. Sururali ya kwanza inakuwa ya fulana, ya pili ya kawaida na ya tatu ya khaki au jeans ili kujikinga na upepo. kisha navaa blausi moja ya fulana ndani na gauni, kisha sweta la fulana lenye kofia (sweater with the hood) na kisha koti zito kabisa juu. Nikitoka nje kufanya kazi sitoki kwa kukurupuka, ni lazima nitumie ubongo, niliambiwa na wazazi wangu wa Kimarekani Dr and Mrs Wilson Trickett "tumia ubongo wako kulinda miguu yako! Au sehemu zako za mwili zilizo mbali na moyo kama vile miguu, mikono na kichwa"

Kingereza alisema "Use your head to protect your legs, au protect your extremities, or your limbs" Kadri kulivyo na tabaka/layers nyingi za nguo mwilini, ndiyo unajikinga na baridi zaidi. Kisha navaa jozi tatu za soksi, na kisha buti za winter zenye manyoya ndani yake. Kisha navaa gloves pamoja na kofia chini ya koti lenye kofia/ hivyo nakuwa na kofia mbili au tatu. Kofia ya kwanza ni ile ya sweta la fulana, ya pili ni ya sweta inaenda yenyewe na ya tatu ni ile ya koti zito. Kusema kwamba nitatembea na gauni bila ya suruali ni kujitakia shida, na hasa wakati huu wa Korona, mapafu yatapata shida, na hutaweza kufanya kazi nje. Kama sasa inabidi kukata kuni za kufanya nyumba iwe na joto wakati wa baridi, inabidi nitembee mazoezi angalau saa moja kila siku, na navyoshugulikia kuhariri machapisho kila baada ya saa au masaa mawili natoka nje. Ukiwa na mtoto mdogo unapojipanga kutoka naye au kwenda kanisani, lazima ujipange vizuri naye na kisha umvishe layers/tabaka kadhaa ya nguo za kuleta jozi. Mikono, kichwa na miguu yetu lazima ilindwe maana ipo mbali na moyo hivyo kusafiri kwa damu kunachukua muda.

Tusiseme tu kwamba mtu asivae Suruali lazima mtu tueleze sababu, kwasababu kwenye Biblia suruali haikuwa vazi la nje la mwanamke au mwanamume. Hakuna mwanamume au mwanamke aliyevaa suruali yenyewe katika Maandiko! Mwanamke anayevaa suruali

yenye blauzi inayofunika vizuri anajistahi kuliko aliyevaa gauni linaloonyesha mgongo, mapaja kwaajili ya sliti au hata makwapa, na sehemu za mwili kwa vile linabana au lina kitambaa kinachoonyesha mwili ndani au matiti, Katika mishono ya vazi la kitaifa, ni jambo ambalo ni la kawaida kabisa kwenye mishono mingi ya

kitaifa kuacha mgongo au kifua wazi au kupasua nguo kwa mtindo unaoitwa slit. Hivyo ni bora mtu akavaa Suruali na kujisitiri kama vile wahindi wanavyovaa na blauzi refu, kuliko sisi tunavyovaa.

Nafikiri utamaduni wetu kwa ajili ya kanga na kaniki umetufanya kuzoea kuacha kifua au mgongo wazi. Ila kama tulivyosema huko mbele mtu anayepaswa kuona uchi wa mtu mwingine ni mzazi wa mtoto mdogo, mwenzi wa mtu aliye naye kwenye ndoa, Daktari kwaajili ya tiba na yule anayesafisha maiti, kituo kikubwa. Ila katika enzi zote au tuseme ujana watu huwa tunashikwa na ugonjwa wa kujionyesha ambao unakwisha mtu akiwa mtu mzima, ila mtu anayeishindania imani waliyopewa Watakatifu, ugonjwa huu haupaswi kumshika akiwa msichana au mama wa miaka 100!
Hebu turudi kwenye kichujio kile kile cha Wafilipi 4:8

"Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya Kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo."

Kwa maneno mengine tumwombe Mungu atupe moyo uliovunjika na kupondeka, hatuwezi kuwa watu wenye shingo ngumu. Hatutaki tuwakwaze watu, lakini hata hivyo

**tukumbuke kuna tamaduni mbali mbali za mavazi tofauti na katika tamaduni zile ambazo watu hawakuvaa kwa heshima wanapomwamini Mungu wanabidi wabadilike na wavae kwa heshima ila sisi hatutakuwa mapolisi wao kuangalia hayo saa yote, kwani hata shuguli zetu tutazifanya saa ngapi? Maana unaweza kuvaa kwa kujifunika kila mahali ila pengine una maisha ya urafiki mbaya**

**na wanaume au wanawake kwa siri. Unaweza kuwa unenda huko ukiwa umevaa ushungi na unalala huko na kufanya mengi, kama vile kuchukua waume wa watu, kufanya njama za kuua watu au kusengenya. Je itasaidia nini basi kama umevaa nguo inayoburuza chini na ushungi ila umejaa uovu moyoni na kuwa na hiana? Naomba nawe utoe maoni yako, maana hapa nasema kama mwanadamu!**

Watoto wa mama mdogo Hajiri huvalia kwa adabu kuliko sisi watoto wa mama mkubwa Sarai, sababu ni ipi basi,

nasi tuna ujumbe wa Masihi ambaye Anakuja hivi karibuni? Japo kitabu hiki kimezungumzia fasheni au mitindo ya miaka 150 iliyopita, inabidi tulinganishe na maisha yetu leo, na kuona pale tunapopaswa kufanya matengenezo ya mavazi ili kuendana na vile Mwenyezi Mungu anataka, na siyo sisi. Maandiko Matakatifu hayana mambo ya zamani! Maagizo Yake ni ya milele! Kigezo kikubwa ni tulapo au tunywapo au tufanyapo japo lolote, tulifanye kwa Utukufu wa Mungu. Rejelea yale mashauri pale juu kwamba "Hakuna mtu yeyote anayepaswa kuuona utupu wetu ila mzazi mtoto anapokuwa mdogo, mtu tuliye naye katika ndoa, daktari kwa ajili ya tiba, na yule anayeosha mwili wakati wa kuzika kaburini," fullstop, kituo kikubwa.

Yaani tunaponunua nguo, tunapovaa asubuhi, tuwaze je, navaa leo ili kumtukuza Mungu, au kuwatukuza madizaina au kujionyesha kwa watu? Hakuna asiyepungukiwa hapa maana sote tunataka watu watuone tunapovaa! Hilo ndiyo jambo la kweli kabisa . Na hilo ni muhimu ili tusivae magunia au nguo

kama za kufukuzia ndege mashambani, nayo pia haitampa Mungu utukufu. Uwiano (balansi), Mungu atatusaidia! Hakuna mwenye uwezo huo isipokuwa YEYE tu!

Wapendwa kitabu hiki ni chetu sote! Maana Masihi Anakuja kuchukua bibi harusi asiye na waa wala kunyanzi. Maneno haya yametuchoma sana, na yanatushawishi tusiwe waongofu tu bali wanafunzi na watu wanaoishi kwa uamsho na matengenezo kila siku, tukiendelea kuwezeshwa na Roho Mtakatifu kubadilisha mitindo yetu ya maisha ili tumpende na kumpendeza Mwenyezi MUNGU, na kuwapenda watu. Katika kukitafsiri tuligundua kwamba utamaduni na enzi za vazi la Matengenezo, inaweza isieleweke vyema na watu wa taifa letu, na hivyo nukuu zingine baada ya kitabu inabidi kurejelewa na picha kuwekwa ili mtu aelewe angalau kwa udogo kile ambacho kilikuwa kikiendelea.

Tumeitwa kumwakilisha Mungu katika maneno, matendo, kula, na kuvaa, ili watu wamwone na kumfuata Yeye, na si sisi wenyewe. Tukimpenda Mungu hatutabaki kama tulivyo kani tutabadilishwa siku kwa siku kwa kumtazama Yeye, tutafanana Naye. Kamwe hatutaabudu mitindo, mavazi, mapambo au chochote zaidi ya Mwenyezi Mungu. Tumesoma mafungu mengi kwenye Maandiko kama vile "Siku hiyo kila mtu atazitupilia mbali sanamu zake za fedha, na sanamu zake za dhahabu, walizojifanyia ili kuziabudu, kwa fuko na popo"-Isaya 2:20 au " Bwana akasema tena, Kwa sababu binti za Sayuni wana kiburi, na kuenenda na shingo zilizonyoshwa, na macho ya kutamani, wakienenda kwa hatua za madaha, na kuliza njuga kwa miguu yao; Basi, kwa hiyo, Bwana atawapiga binti za

Sayuni kwa pele za utosini, na Bwana ataifunua aibu yao. Siku hiyo Bwana atawaondolea uzuri wa njuga zao, na kaya zao; na pete za masikio, na vikuku, na taji zao; na dusumali, na mafurungu, na vitambi, na vibweta vya marashi, na matalasimu; na pete, na azama, na mavazi ya sikukuu, na debwani; na shali, na vifuko; na vioo vidogo, na kitani nzuri, na vilemba, na utaji. Hata itakuwa ya kuwa badala ya manukato mazuri kutakuwa uvundo, na badala ya mishipi, kamba; na badala ya nywele zilizosukwa vizuri, upaa; na badala ya kisibau, mavazi ya kigunia; na kutiwa alama mwilini kwa moto badala ya uzuri." Isaya 3:16-21. au Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; bali kuwe utu wa moyoni usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na kuwatii waume zao. Kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akamwita Bwana; nanyi ni watoto wake, mfanyapo mema, wala hamkutishwa kwa hofu yoyote. 1 Pet 3:3-6

Nguvu ya injili hutoka ndani ya moyo ndiyo humbadilisha mtu, nayo ni endelevu kadri tunavyoendelea kukua katika

Kristo, vitu vingine mtu hawezi kutuambia bali tutajikuta tunaviacha wenyewe kwa furaha bila hata ya kubishana na mtu, kwani tutagundua kuwa tunaokolewa kwa neema na si kwa mavazi au mapambo yetu. Ni vigumu kumwekea mtu kigezo, na akakifuata kwa moyo wake wote. Ni kawaida ya binadamu kujionyesha na kutaka watu wamwangalie ili kuona uzuri wake, elimu, ujuaji, utajiri wake nk. Hivi vyote vinaturudisha nyuma kiroho kwani kwa desturi, huwa tunapenda kuabudu nafsi zetu, tupende au tusipende kulimeza hili, huu ndio ukweli wenyewe ulivyo. Basi, zamani zile za ujinga Mungu alijifanya kama hazioni; bali sasa anatuagiza watu wote wa kila mahali tutubu. Kwa maana ameweka siku atakayotuhukumu walimwengu kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua; Naye ametupa watu wote uthabiti wa mambo haya kwa kumfufua Yesu katika wafu Matendo 17:30, 31. Tunaishi wakati wa maarifa mengi, na Maandiko Matakatifu ndiyo kitabu kinachouzika duniani kuliko kitabu kingine kwa miaka takribani miaka 3000 hivi, toka Musa alipoandika na watu wakanakili kwa mkono na hata watu wa dini za mashariki wametuonyesha, mishono ya mavazi ambayo sisi tulio Wakristo tunapaswa kuyatilia makini, ili tusimwaibishe Mungu.

Mara nyingi tunapozungumzia uwakili, huwa tunasema uwakili wa muda, fedha, afya nk, ila uwakili ni mitindo yetu ya maisha ni jumla ya mambo yote. Uwakili ni kufanana na Kristo, kuiga tabia Yake (emulate Him), Wema Wake, kuilinda injili ambayo tumepewa sisi ambao

ni vyombo vya udongo.

## KWANINI TUNAVAA NGUO?

Sababu peke yake ya sisi kuvaa nguo ni MWENYEZI MUNGU alituambia baada ya dhambi, kwamba “sasa Mimi sikuviki na utukufu Wangu, hebu ufiche aibu yako, Sisi si mapolisi wa dunia wa kuwaambia watu wavae nini, vito gani wanapaswa kuviweka, wale nini, wazungumzaje, waimbe nyimbo zao namna gani, au wakae nyumba ya namna gani etc

**KICHUJIO CHETU** wote wenye mwili ni Kile Mungu amekitoa baada ya maagizo YAKE, yaani kile cha Wafilipi- 4:8 Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yoyote yaliyo ya staha, yoyote yaliyo ya haki, yoyote yaliyo safi, yoyote yenye kupendeza, yoyote yenye sifa njema; ukiwapo wema wowote, ikiwapo sifa nzuri yoyote, yatafakarini hayo. [9] Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi." Haruni kama mwanamume aliambiwa atakapopanda ngazi kwenye madhabahu ya kukutania avae kaptura ndani, mapaja yake yasionekane, asije akakatiliwa mbali. Hiki kinaonyesha kwa wale waliotambulishwa Kidogo kwenye Maandiko kama sisi, tumeanza safari endelevu ya kuchuja mambo mengi kwa uwezo wa Mungu kupitia, upendo, Maandiko, maombi, Roho Mtakatifu, hekima, na uzoefu bora. Hakuna kesi zinazofanana-fanana, sisi si mapolisi wa wengine ila pia sisi si mbwa wasiobweka! Tutajuaje tofauti? Kwa kuomba, na

upendo kwa watu hawa. Hatuwezi kuwakenulia meno kama watapata shida, na hatuwezi kuwa polisi wao. Tunachoomba ni hekima tu kutoka kwa Mungu katika kila hali tunayokutana nayo, tunahitaji Mshauri wa Ajabu. MUNGU atusaidie kujibadilisha sisi wenyewe zaidi ya mtu yoyote! Maana tunawajibika kwetu wenyewe zaidi ya kwa mtu mwingine. Ila watu tunaofanya nao urafiki, tukiwashauri kwa upendo tunapoona wanahitaji ushauri, litakuwa jambo bora. Ila inakuwa rahisi zaidi kumshauri mtu ambaye ni rafiki. Usigombane na watu, fanya haya kwa upendo, maana unaweza ukashinda vita ila upoteze roho, au ukashinda pambano, ila ukashindwa vita.

Ezekieli 3 Yasema, Akaniambia, Mwanadamu, haya! Waendee wana wa Israeli ukawaambie Maneno Yangu. Maana wewe hukutumwa kwa watu wa maneno mageni, ama wa lugha ngumu, bali kwa nyumba ya Israeli; si kwa watu wa kabila nyingi wenye maneno mageni, na lugha ngumu, ambao huwezi kufahamu maneno yao. Bila shaka, kama ningekutuma kwa watu hao, wangekusikiliza. Bali nyumba ya Israeli hawatakusikiliza wewe; kwa kuwa hawanisikilizi Mimi; maana nyumba yote ya Israeli wana vipaji vigumu, na mioyo yenye ukaidi. Tazama, nimeufanya uso wako kuwa mgumu juu ya nyuso zao, na kipaji cha uso chako kuwa kigumu juu ya vipaji vya nyuso vyao.

Sisi si yaya (babysitter) wa ndugu zetu au mlinzi kama Kaini alivyosema bali wakati huo huo ni yaya, kwa namna gani basi? Jadili hili
Mchungaji Kisaka alipenda kutuambia miaka ya 80 kama Chaplain wetu wanafunzi wa Dar "Tukiwa tunapaa kwenda mbinguni na tuko mawinguni na kisha tukamwona mtu amevaa bangili, tutasema Bwana Yesu sitisha msafara maana kuna mtu hapa amevaa bangili, mrudishe duniani!" Sisi si kipimo cha mtu, hata Petro aliambiwa na Yesu wakati anamsengenya Yohana, aache umbeya wa kuhusianisha watu wengine, wakati Bwana alikuwa akizungumza naye. Mungu aliumba vito na anapenda sana uzuri, na mtu akivaa Scarf ya dola 100 ili kujionyesha. au avae suti ya dola 5000 au akaweka dola 1000 masikioni mwake basi ni yeye kujiuliza kama hivi vitu anavaa ili kumpa Utukufu Mungu au anajionyesha na kushindwa kusaidia masikini kama Nebukadneza kwenye Daniel 4. Sasa mtu huyu atajaza jedwali mwenyewe. Je, unatumia pesa kwa mavazi zaidi ya Injili kwa kuwaambia watu Masihi anakuja? Ila kama kanisa kuna vitu wakati tumebatizwa tumeambiwa viwe sare/Uniform ili tusiwakwaze au kuwakanganya watoto wetu au watu wa karibu. Kama Kanisa tumesema kwamba kuweka mali zetu au kuzionyesha masikioni, au kwenye mikono, au shingoni au miguuni siyo jambo, jema au la hekima, hivyo lisifanywe, na pia laweza

kuwachanganya sana watoto wetu au wale wachanga kwa imani. Sasa tujiulize kama vitu hivi ni vya muhimu sana kwetu? Kila mtu anapaswa kuchunguza moyo wake na kuonya vile anavyopaswa kuviacha au kusahihisha. Sisi hatuna kipimo yaani Spiritualmeter au Christometer, ila kwa mambo machache tumepewa kazi ya kukagua matunda ila tusipende kuyakagua matunda saa zote Mathayo 7:15-20

**Ni vyema tuseme kuwa katika enzi zote au pengine tuseme ujanani, watu hushikwa na ugonjwa wa kujionyesha ambao unakwisha mtu anapofikia utu uzima, ila mtu anayeishindania imani waliyopewa Watakatifu, ugonjwa huu haupaswi kumshika akiwa msichana au mama wa miaka 100!**

Mungu awabariki mnaposoma kitabu hiki, kwani hakuna mwanadamu mwenye jibu la kila swali, ila tukitumia vigezo vilivyoandikwa mwenye kitabu hiki, hakika hatutafeli. Nasi siku moja tutavikwa taji na vito vyenye thamani, na Yule aliye wa Thamani Kupita vyote mbinguni na duniani, Ndilo ombi langu

Masihi Anarudi. Roho na Bibi arusi waseme, “Njoo!” Kila mtu asikiaye hili, na aseme, “Njoo!” Aliye na kiu na aje; anayependa, na achukue maji ya uzima bila malipo.Amina. Njoo Bwana Yesu!Tunawatakieni nyote neema ya Bwana Yesu. MARANATHA Wapendwa wa
BWANA! Amina

Walei Uhamishoni, Ughaibuni, Mtandaoni na Majumbani
Grace Momadi-Masaka

*Muhtasari*

Kitabu cha Kingereza cha kielektroniki cha mada hii kimetolewa na Ellen G. White Estate. Kimejumuishwa katika mkusanyiko mkubwa wa Vitabu vya Mtandaoni bila malipo kwenye Ellen G. White na kwenye Tovuti ya Ellen G. White

## KUHUSU MWANDISHI

Ellen G. White (1827-1915) anachukuliwa kuwa ndiye Mwandishi ambaye maandishi yake yametafsiriwa kwa wingi zaidi kwa waandishi wote wa Marekani, kazi zake zimechapishwa katika lugha zaidi ya 160. Aliandika zaidi ya kurasa 100,000 (laki moja) zenye mada za kiroho na za kawaida . Akiongozwa na Roho Mtakatifu, alimwinua Yesu na kuwaelekeza watu kwenye Maandiko Matakatifu kuwa Ndiyo msingi wa imani ya mwanadamu..

"Dada zangu, kuna haja ya matengenezo ya mavazi miongoni mwetu. Kuna makosa mengi katika mitindo ya sasa ya mavazi ya kike."

Kauli ya D. E. Robinson kuhusu mazingira ya kihistoria ya Wito wa Ellen White wa matengenezo na kanuni za mavazi za wakati huo, zinaweza kuwa tofauti na za leo.

Hii imetolewa kutoka katika kisa cha Ujumbe wetu wa Afya (The Story of Our Health Reform): Sura ya 9, 10, na 13.

Kwa maneno haya Bibi White alianzisha makala yake ya sita na ya mwisho kuhusu "Magonjwa na Sababu Zake," katika mfululizo wenye kichwa "Jinsi ya Kuishi," iliyotolewa na kuchapishwa mwanzoni mwa mwaka 1865.

YALIYOMO

Taarifa kuhusu Kitabu hiki ........................................................5

Utangulizi ..........................................................................8

Soma Nukuu za Shuhuda za Gombo la Kwanza na Gombo la Nne mwisho wa kitabu ili kukupa historia ya kuelezea vazi la matengenezo la Marekani, yaani mshono uliobuniwa (Model) na Sketi za Hoops-Maelezo ya kusaidia kuelewa kilichokuwa kinaendelea.

Sura ya 1—Mitindo ya Sare Haihitajiki (uniform siyo lazima, siyo kila mtu lazima avae sawa na mwingine) 9

Sura ya 2—Isiwe Kweli Yetu ya Sasa..................................... 10

Sura ya 3—Masuala Hai Yanayopaswa Kutimizwa.......................... 11

Sura ya 4—Wengine Hawatatii.................................................12

Sura ya 5—Jaribio la Kweli.............................................................. 14

MAKALA MENGINE YANAYOHUSU MAVAZI-TUSAIDIANE KUTAFSIRI ILA MADA (TOPIC) YA MAVAZI NI MTU BINAFSI KUOMBA UONGOZI WA MUNGU

## Utangulizi

Kwa kujibu maswali ambayo yamenijia hivi karibuni kuhusiana na kurudia tena kuhusu kuvaa vazi la matengenezo, ningependa kusema kwamba wale ambao wamekuwa wakilitibuatibua somo hili au kufanya kampeni kuhusiana nalo, wanaweza kuhakikishiwa kwamba hawaongozwi na Roho wa Mungu kuhusu jambo hilo.

Bwana hajaonyesha kuwa ni wajibu wa dada zetu kurejea kwenye vazi la matengenezo (Lilikuwa ni vazi rasmi, lenye mshono mahiri, ambalo

walifikiri walipaswa kulifuata nalo liliitwa vazi la Marekani la Matengenezo).

Matatizo ambayo tumekwisha kukutana nayo tusiletewe tena hata mara moja. Hakuna haja ya kuchepuka na kuelekea kwenye aina moja ya vazi. Mambo mapya na ya kushangaza yatatokea daima, ili kuwaongoza watu wa Mungu katika msisimko wa uongo, uamsho wa kidini, na udadisi wa aina fulani; lakini watu wetu hawapaswi kufanyiwa mitihani au vigezo vyoyote ambavyo vinatokana na uvumbuzi wa mwanadamu na hivyo kuleta mabishano katika kila mstari au mada.

Ushauri wa mtindo wa vazi la matengenezo la zamani ulithibitisha vita kwenye kila hatua. Kwa baadhi ya watu hapakuwa na usawa, yaani mavazi hayo hayakufanana na pia hawakupenda maandalizi ya vazi hilo, na kwa wale waliookataa kulipokea vazi hilo walisababisha mgawanyiko na mafarakano. Kwa hivyo kazi ya Mungu iliaibishwa. Kwa sababu kile kilichotolewa kama baraka kiligeuzwa kuwa laana, na jukumu la kutetea vazi la matengenezo" liliondolewa.

Kuna baadhi ya mambo ambayo yalifanya vazi la matengenezo" kuwa baraka.

Kwasababu wakati huo wa miaka ile ya 1800, kulikuwa na sketi za ajabu za hoops au magauni ya hoops ambayo yalibana kiunoni na kufanya sketi ya mwavuli iliyokuwa ndefu na hata kuburuza njia (google); Nguo hii ndiyo ambayo Ilikuwa kwenye mtindo/fasheni ya wakati huo, hili haliwezi kuwa shida ya wakati huu; wala uvaaji wa sketi ndefu, zinazofagia uchafu wa mitaani, haziwezi kuwa sehemu ya mabishano ya wakati huu. Lakini katika miaka ya hivi karibuni mtindo wa vazi ulio mzuri na wa busara zaidi umepitishwa na dunia, na huo hauna vipengele vile vinavyochukiza au kupingwa; na kama dada zetu wanataka kushona mtindo wao wa nguo

kutoka katika mifano hii iliyo sahili, rahisi na wazi, Bwana hatakuwa amevunjiwa heshima kwa kufanya hivyo.

(Leo pia tunakabiliwa na shida za mitindo, hivyo kichujio cha Wafilipi 4:8 ni muhimu)

***Wafilipi* 4: 7**

**Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu**
**na nia zenu katika Kristo Yesu.** 8 ***Hatimaye, ndugu zangu, mambo yoyote***
***yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote***
***yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo***
***wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo.*** 9 **Mambo**
**mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu,**
**yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi.**

(MAELEZO YA mwisho wa kitabu YATAFAFANUA ZAIDI KUHUSU MAVAZI AMBAYO YAMESIMULIWA KWENYE kitabu hiki, hili ni muhimu kwa watu wa kizazi hiki na wenye utamaduni tofauti na ule wa Marekani- Maelezo hayo YANATOKA KWENYE SHUHUDA Gombo la Kwanza na Gombo la NNE na yamerejelewa kwenye kitabu hiki kwa ufupi)

# SURA YA 1—MTINDO WA SARE KWA WOTE HAUHITAJIKI

Wengine wamedhani kwamba mtindo wa mavazi wa shati na vazi la blauzi ya zamani iliyotajwa ndani ya S h u h u d a 4:640 ulikuwa ni kielelezo ambacho watu wote walipaswa kufuata (angalia mwisho wa kitabu tumebandika nukuu hizo za Mavazi za gombo la Nne la Shuhuda). Lakini hii haipo hivyo, lakini

Pateni/mshono wa vazi rahisi kama hili unapaswa kutumika. Hakuna mtindo wowote haswa wa vazi ambao nimepewa kuwa kama sheria kamili (na kali) ya kuwaongoza watu wote katika mavazi yao. Ikiwa dada zetu wataona ni lazima kwao kuchukua vazi linalofanana kwao wote (sare kwa wote), mabishano yangetokea, na wale ambao akili zao zinapaswa kutolewa kikamilifu kwa kazi ya ujumbe wa malaika wa tatu wangetumia muda wao kufanya vita vikali juu ya mavazi, na kupuuzia uchamungu wa ndani, ambalo ni pambo la upole na roho ya utulivu, iliyo ya thamani kuu machoni pa Mungu.

## SURA YA 2—ISIWE KWELI YETU YA SASA



Swala la mavazi sio Ukweli wetu wa sasa. Kujihusisha na suala hili kwa sasa kungemfurahisha adui. Shetani anafurahi pale

akili inapoelekezwa kwa somo lolote ambalo linaweza kujenga mgawanyiko wa hisia, na kusababisha watu wetu kuwa katika mabishano. Ninawasihi watu wetu waenende kwa uangalifu na kwa

umakini mkubwa mbele za Mungu. Fuateni mtindo wa mavazi unaoendana na kanuni za afya. Hebu dada zetu wavae kwa usahili, kama wengi wanavyofanya, wakiwa na mavazi yenye kitambaa kizuri, na cha kudumu, kinachofaa kwa zama hizi, na tusiruhusu swala la mavazi lijaze akili zetu. Dada zetu wanapaswa kuvaa kwa usahili (mavazi rahisi). Wanapaswa kuvaa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu na kiasi. Upeni ulimwengu kielelezo hai cha kujipamba kwa utu wa ndani kwa neema ya Mungu. Jiwekeni chini ya nidhamu ya Mungu mbele ya walio hai, mkisalimisha nia zenu chini ya mivuto inayounda tabia njema.

Angalizo: Katika barua ya Ushauri iliyoandikwa wakati huu, Bibi White alihimiza: "Fuata desturi ya mavazi katika matengenezo ya afya, lakini si kwa kuanzisha tena mavazi mafupi na suruali isipokuwa mna Neno kutoka kwa Bwana kwa ajili yake."— Barua ya 19, 1897 .

## SURA YA 3—MASUALA YA SASA YANAYOPASWA KUZINGATIWA

11 11

Tunakaribia mwisho wa historia ya ulimwengu huu. Tuko karibu kukabiliana uso kwa uso na migogoro mikubwa, dhoruba

za mifarakano, ambayo ni wachache wanayo kwenye mafikra yao; na wakati wetu wote na nguvu ya mawazo yetu vinapaswa kuwekezwa kwenye masuala nyeti ya maisha yaliyo mbele yetu. Mungu ana

mitihani katika zama hizi, nayo ipo kutupima kwa uwazi na bila makosa. Tumechelewa sana kwa sasa kuweka shauku zetu kwenye majaribio yoyote yanayofanywa na mwanadamu. Mtihani mkubwa kwa wakati huu ni juu za amri za Mungu kumi, na hasa Sabato, na hakuna kitu kinachopaswa kuuteka umakini wetu na mioyo yetu na kututoa katika maandalizi yanayohitajika kukutana na mtihani huo. Watu wa Mungu watakutana na mtihani wao wote na katika kile kipimo wanachoweza kubeba. Swala la Sabato ni mtihani ambao utakuja kwa wanadamu wote wa dunia hii. Hatuhitaji kitu chochote kuingilia kwa sasa, ili kuwajaribu watu wa Mungu, kwani hilo litawazidishia ugumu wa mtihani walio nao.

Ebu dada zetu walitii Neno la Mungu kwa uangalifu, wao wenyewe. Usianze kazi ya matengenezo hadi umeamua kufanya hivyo. Kamwe huwezi kuubadilisha moyo. Kuwa na mtindo tofauti wa mavazi hakuwezi kufanya hivyo. Jambo lililo gumu ni kwamba, kanisa linahitaji kuongoka kila siku. Hapo kuna mambo mengi yatakayokuja kuwajaribu watu hawa maskini, waliodanganyika, mbilikimo wa kiroho, wanaopenda ulimwengu.
Watu watakuwa na majaribu ya kina sana. Hebu pasiwepo na majaribio yanayofanywa na mwanadamu, kwa maana Mungu

amejitayarisha kuwathibitisha kwa majaribio/mitihani. Ikiwa watazingatia mawaidha na maonyo Yake, na kuwa wanyenyekevu kwa nafsi zao mbele Zake, hebu na waache Yeye awe kiini cha ibada yao, Yeye atawapokea kwa neema Yake.

Utendaji wa Roho wa Mungu utaonyesha mabadiliko kwa nje. Wale wanaothubutu kutotii kauli hizi zilizovuviwa na Roho Mtakatifu na zilizo wazi kabisa, hawatasikiliza juhudi zozote za kibinadamu zinazofanywa kuwashawishi kuvaa mavazi nadhifu, sahili, yasiyo na mapambo,na yanayofaa, ambayo hayatawafanya kwa njia yoyote waonekane tofauti sana na wa kipekee. Wataendelea kujifunua kwa kuzionyesha rangi zao kwa ulimwengu.

## SURA YA 4—WENGINE HAWATATII

Kuna wale ambao hawana mpango wa kuurudia upendo wao wa kwanza. Wao hawaachi kuzifanya nafsi zao kuwa sanamu (mungu, yaani wanajiabudu wenyewe na hata kupitia mavazi). Licha ya nuru yote ya Neno ya Mungu inayoangazia kwenye njia zao, hawayatatii maelekezo Yake Bwana. Nao wanaendelea kufuata ladha zao wenyewe, na kufanya vile watakavyo. Hawa wakina dada wanatoa mfano mbaya kwa vijana, na kwa wale ambao ni wapya katika imani, kwa maana wanaona tofauti ndogo kati ya mavazi yao na yale ya walimwengu.

Kwa wale wanaofanya nafsi zao kuwa sanamu, hakuna majaribio ya kibinadamu yanapaswa kuwasilishwa kwao, kwa kuwa yatawapa tu udhuru na mwishowe watatumbukia katika ukengeufu, kwa vile hawamjui Yule ambaye wanamtumikia. Maarifa na nguvu vinatoka kwa Mungu. Watu wale wenye hatia kwa ujinga wao wenyewe, ni lazima wajifunze hali yao. Lazima tuwe na subira, na uvumilivu na sio kushindwa/kufeli au kukata tamaa, kwa

kuwa Mungu ana mikakati Yake aliyokwisha kuipanga. Tukiwa tumelemewa na kufadhaika, ila tukangojea kwa kujisalimisha kwa subira, Msaidizi wetu Yule asiyeonekana atakuwa anafanya kazi tusiyoiona kwa macho, na atatimiza

kwa Majaliwa au Mpango Wake, na kisha matukio yatatimia ama kwa kazi ya matengenezo, au kwa kutawatenganisha washiriki hawa waliongoka nusu nusu na wale wanaopenda ulimwengu kutoka kwa waumini waaminifu. Bwana anajua kila kitu kuhusu kesi zetu, na jinsi ya kukabiliana na kila mmoja. Hakika hekima yetu ina mipaka, wakati hekima isiyo na kikomo ya Mungu inafahamu mwisho tangu mwanzo. Muda wetu wote wa majaribio ni mfupi sana. Kazi fupi itafanywa duniani. Majaribio ya Mungu Mwenyewe yatakuja; Uthibitisho Wake utakuwa mkali na wa haki. Hebu kila nafsi ijinyenyekeze mbele za Mungu, na kujitayarisha kuhusu kile kinachotujia.

Hebu wakina dada hawa wenye dhamiri kali ambao wameingia kwenye kazi ya matengenezo juu ya mavazi, watembee kwa uangalifu, na wafanye kazi kwa njia ambayo italingana na mzigo wa ujumbe wa wakati huu. Kujisalimisha kwa moyo, nafsi na akili katika utiifu kwa

amri ya Mungu ni kama uzi wa dhahabu, unaofunga vitu vya Mungu vya thamani na kufichua thamani yake wakati wa majaribio.

Kwa hiyo nawaambia madada zangu, Msibishane katika jambo lolote linalohusu mavazi ya nje, lakini hakikisha kwamba una mapambo ya ndani ambayo ni roho ya upole na utulivu. Hebu wote wanaokubali ile Kweli waonyeshe kwa uwazi rangi zao halisi. Sisi tumewekwa kuwa tamasha kwa ulimwengu, kwa malaika, na kwa wanadamu. Uongo katika mwenendo na kujistahi, adabu yenye dhihaka, inaweza kuonyeshwa kwa mavazi ya nje; huku moyo ukiwa ukiwa na hitaji kubwa la mapambo ya utu wa ndani. Simama imara daima na kujisalimisha kwenye nuru ya ile Kweli.

## SURA YA 5—JARIBIO LA KWELI

Usiangalie pande zote ili kuona kama hakuna majaribu yanayoweza kuletwa juu ya watu wa Mungu. Mungu ametoa mtihani-Sabato ya amri ya Nne. "Hakika mtazishika Sabato Zangu; Ni ishara baina Yangu na nyinyi katika vizazi vyenu vyote; ili mpate kujua ya kuwa Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye ninyi.... Kwa hiyo wana wa Israeli wataishika Sabato, kuitunza Sabato katika vizazi vyao, ni agano la milele. Ni ishara kati Yangu na wana wa Israeli milele; kwa maana katika siku sita Bwana alizifanya mbingu na nchi, akaibariki siku ya saba, akastarehe na kupumzika" [Kutoka 31:13-17].

Wote wanaoleta moyo uliowekwa wakfu kwa Mungu kwenye utunzaji wa Sabato, watapata kujua kwamba siku ambayo Mungu ameitakasa ni zaidi ya vile walivyokuwa wanawaza hapo kabla. "Mimi Ndimi Bwana niwatakasaye" (Kutoka 31:13). "Kama ukigeuza mguu

wako usihalifu Sabato, usifanye anasa yako siku ya utakatifu Wangu; ukiita Sabato siku ya furaha, na siku takatifu ya Bwana yenye heshima; ukiitukuza, kwa kutokuzifanya njia zako mwenyewe, wala kuyatafuta yakupendezayo, wala kusema


12

maneno yako mwenyewe; ndipo utakapojifurahisha katika Bwana; Nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha Bwana kimenena hayo. " (Isaya 58:13, 14 .— Ms 167, 1897 .

## MAELEZO ZAIDI KUHUSU MAVAZI KUTOKA SHUHUDA GOMBO LA KWANZA NA LA NNE

Hakuna nafasi inayopaswa kutolewa kwa wasioamini kutukana imani yetu. Tunachukuliwa kuwa wa kawaida na wa kipekee hivyo hatupaswi kuchukua kusudi la kuwaongoza wasioamini kutufikiria zaidi ya vile imani yetu inavyotutaka tuwe.{1T 420.2}

Baadhi ambao wanauamini Ukweli wanaweza kufikiria kuwa inafaa zaidi kwa akina dada kuiga vazi la tamaduni za Marekani, lakini ikiwa mavazi hayo yangelemaza ushawishi wetu miongoni mwa wasioamini ili tusiweze

kupata urahisi wa kuwafikia, hatupaswi kwa namna yoyote kuiga, ingawa tulipata mateso mengi kama matokeo yake. Lakini wengine wanadanganywa kwa kufikiria kuwa kuna faida nyingi ya

kupokea vazi hili. Ingawa inaweza kudhihirisha faida kwa wengine, kwa wengine ni jeraha. [Angalia Kiambatanisho.] {1T 421.1}

Niliona kwamba agizo la Mungu limebadilishwa, na maagizo Yake maalum hayazingatiwi, na wale wanaoiga vazi la Amerika. Nilirejelewa kwenye Kumbukumbu la Torati 22: 5: "Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako." Mungu asingependa watu Wake wapokee kile kinachoitwa mavazi ya matengenezo. Ni mavazi yasiyo na adabu, hayafai kabisa kwa wafuasi wa Kristo wanyenyekevu. {1T 421.2}

Kuna kuongezeka kwa tabia ya kuwa na wanawake katika mavazi yao na muonekano wao karibu sawa na jinsia nyingine iwezekanavyo, na kutengeneza mavazi yao kama ya wanaume, lakini Mungu anaitamka kuwa chukizo.

"Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; 1 Timotheo 2: 9. {1T 421.3}

 12

Wale ambao wanahisi wameitwa kujiunga na vuguvugu hiyo wakidai haki za mwanamke nakile kinachoitwa matengenezo ya mavazi wanaweza pia kukata uhusiano wote na ujumbe wa malaika wa tatu. Roho inayohudumia moja haiwezi kupatana na hiyo nyingine. Maandiko yako wazi juu ya uhusiano na haki za wanaume na wanawake. Wafuasi wa roho za umizimu wamepitisha mtindo huu wa mavazi. Waadventista wa Sabato, ambao wanaamini katika kurejeshwa kwa karama, mara nyingi hujulikana kama washirika wa roho ya umizimu. Acha waige desturi hii, na ushawishi wao umekufa. Watu wangewaweka katika kiwango cha washirika wa roho ya umizimu na wangekataa kuwasikiliza. {1T 421.4}

Pamoja na kile kinachoitwa matengenezo ya mavazi (Dress reform) kuna roho ya kukosa heshima na ujasiri kwa kuzingatia mavazi. Unyenyekevu na uhifadhi huonekana kuondoka kwa wengi wanapoiga mtindo huo

wa mavazi. Nilioneshwa kwamba Mungu angependa tuchukue hatua thabiti na za makusudi. Wadada wanaoiga desturi za mavazi ya Marekani na wataharibu mvuto wao na wawaume zao. Watakuwa wenye vinara vya kuongoza kwa ubaya na dhihaka . Mwokozi wetu anasema: "Ninyi ni

nuru ya ulimwengu." "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, ili wapate kuona matendo yenu mema, na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni." Kuna kazi kubwa kwetu ya kufanya ulimwenguni, na Mungu hatatutaka tuchukue shauri la kupunguza au kuharibu mvuto wetu kwa ulimwengu {1T 422.1}

**Sura ya 83 ya Gombo la Kwanza la Shuhuda - Matengenezo Katika Mavazi**

Ndugu Wapendwa kaka na Dada: rai yangu kwa kutaka usikivu wenu tena juu ya mada ya mavazi ni kwamba baadhi wanaonekana kutoelewa kile nilichoandika hapo awali; na juhudi hufanywa, labda na wale ambao hawataki kuamini kile nilichoandika, kufanya machafuko katika makanisa yetu juu ya mada hii muhimu. Barua nyingi zimetumwa kwangu, zikibainisha changamoto, ambazo sikupata nafasi ya kuzijibu; na sasa, kujibu maswali mengi, ninatoa maelezo yafuatayo, ambayo bila shaka yanatumainiwa kuwa suluhisho la daima la mada hii, kwa


12

kadri ushuhuda wangu unavyohusika. {1T 456.1}

Wengine wanadai kwamba kile nilichoandika katika *Ushuhuda kwa Kanisa* Namba 10 hakikubaliani na

 12

ushuhuda wangu katika kitabu kinachoitwa, *Jinsi ya Kuishi (How to Live)*. Ziliandikwa kutoka mtazamo mmoja, hivyo sio mitazamo miwili inayopingana, kama wengine wanavyoweza kudhani; ikiwa kuna tofauti yoyote, ni katika namna tu ya kujieleza. Katika Ushuhuda wa Kanisa Namba 10 nilisema kama ifuatavyo: {1T 456.2}

"Hakupaswi kuwepo tukio litakalotumiwa na wasioamini kuishutumu imani yetu. Tunachukuliwa tusio wa kawaida na wa pekee, na hatupaswi kuwa chanzo cha kuwaongoza wale wasioamini kutufikiria zaidi ya vile imani yetu inavyotutaka tuwe. Wengine ambao wanauamini Ukweli wanaweza kufikiri kwamba ingekuwa vyema zaidi kwa akina dada kuiga mavazi ya Marekani (American Costume, vazi la taifa), lakini ikiwa mtindo huo wa mavazi ungedhohofisha mvuto wetu kwa wasioamini na kupelekea kushindwa kupata urahisi wa

kuwafikia, basi hatupaswi kuuiga kwa namna yoyote, ingawa matokeo yake yalitutaabisha sana. Lakini wengine wamedanganyika kwa kudhani kuna faida nyingi wanazoweza kupata kwa kuiga

 12

mtindo huu wa mavazi. Japo unaweza kuwa na faida kwa baadhi, una madhara kwa wengine. {1T 456.3}

"Niliona kwamba agizo la Mungu limebadilishwa, na maagizo Yake maalum hayazingatiwi, na wale wanaoiga mtindo wa mavazi ya Marekani (Vazi la taifa-America costume). Nilirejezwa kwenye Kumbukumbu la Torati 22: 5: "Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwanamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana, Mungu wako."" Mungu asingependa watu Wake wajiingize katika kile kijulikanacho kama matengenezo ya mavazi. Ni mavazi yasiyo na adabu, na yasiyofaa kabisa, kwa wafuasi wanyenyekevu wa Kristo kujistiri. {1T 457.1}

"Kuna ongezeko la mazoea kwa wanawake katika mavazi yao na muonekano wao kushabihiana kwa karibu sana na ya jinsia nyingine, na kutengeneza mavazi yao

katika mtindo kama wanaume, lakini Mungu anatamka kuwa ni chukizo. "Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujistiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi;" 1 Timotheo 2: 9. {1T 457.2}

"Wale wanaohisi wameitwa kujiunga na vuguvugu la kudai haki za mwanamke na kile kinachoitwa matengenezo ya mavazi wanaweza pia kukata uhusiano wote na ujumbe wa malaika wa tatu. Roho amhudumiae huyu hawezi kuwa katika maelewano na mwingine. Maandiko yako wazi juu ya uhusiano wa haki za wanaume na wanawake. Wana umizimu kwa kiasi fulani wamepitisha mtindo huu wa kipekee wa mavazi. Wadventista wa Sabato, ambao wanaamini katika kurejeshwa kwa karama, mara nyingi hujulikana kama wana umizimu. Watakapoiga mtindo huu wa mavazi, mvuto wao utakuwa umekufa. Watu wangewafananisha na wanaumizimu na wangekataa kuwasikiliza. {1T 457.3}

"Kutokana na kile kinachoitwa matengenezo ya mavazi kumekuwa na roho ya purukushani na ujasiri ili kuendana na mavazi. Adabu, uungwana na kujisitiri vinaonekana kutoweka kwa watu wengi pindi wanapoiga

mtindo huo wa mavazi. Nilioneshwa kwamba Mungu angependa tuchukue mwelekeo thabiti na unaoelezeka. Endapo kina dada wataiga mitindo ya vazi la Amerika, basi watauharibu mvuto wao wenyewe na ule wa waume zao. Wangekuwa

msemo wa kejeli na dhihaka. Mwokozi wetu anasema: "Ninyi ni nuru ya ulimwengu." "Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu Aliye mbinguni." Kuna kazi kubwa kwetu ya kufanya ulimwenguni, na Mungu hatatutaka tuhafifishe au kuharibu mvuto wetu kwa ulimwengu. "{1T 457.4}

Yaliyotangulia nilipewa kama karipio kwa wale ambao wamependa kufuata mtindo wa mavazi yanayofanana na yale ambayo huvaliwa na wanaume; lakini wakati huo huo nilioneshwa ubaya wa mtindo wa kawaida wa mavazi ya mwanamke, na kurekebisha haya, pia nilitoa yafuatayo yaliyopatikana katika Ushuhuda kwa Kanisa, Nambari 10: {1T 458.1}

"Hatufikirii kulingana na imani yetu kuvaa kwa kufuata mtindo wa vazi la Marekani (American Dress), kuvaa sketi za hoops, au twende kwa kupita kiasi

katika kuvaa nguo ndefu ambazo zinafagia njia za barabarani na mitaa. Ikiwa wanawake wangevaa nguo zao ili zisisafishe uchafu wa mitaa, inchi moja au mbili juu ya ardhi, mavazi yao yangekuwa ya adabu, na yangehifadhiwa kwa usafi na kwa urahisi zaidi, na

 12

kuvaliwa kwa muda mrefu. Mavazi kama hayo yangefaa kulingana na imani yetu. " {1T 458.2}

Sasa nitatoa dondoo kutoka katika kile nilichosema mahali pengine juu ya mada hii: {1T 458.3}

"Wakristo hawapaswi kujishugulisha mno ili tu wawe maonyesho ya vituko kwa kuvaa tofauti na ulimwengu. Lakini ikiwa, wakati wa kufuata imani zao za wajibu kwa kuzingatia mavazi ya heshima na afya, watajikuta wametoka nje ya mitindo (zilipendwa, enzi ya mawe au old fashion), hawapaswi kubadilisha mavazi ili kufanana na ulimwengu, lakini wanapaswa kuonesha uhuru mkamilifu na ujasiri wenye maadili yaliyo sahihi, ikiwa ulimwengu wote unatofautiana nao. Ikiwa ulimwengu utaleta mavazi yenye adabu, rahisi, na yenye afya, ambayo ni kwa mujibu wa Biblia, haitabadilisha uhusiano wetu na Mungu au ulimwengu kufuata mtindo kama huo wa mavazi. Wakristo wanapaswa kumfuata Kristo na

kufanya mavazi yao yalingane na Neno la Mungu. Wanapaswa kuachana na mienendo ya kupitiliza (extreme). Wanapaswa kwa unyenyekevu kufuata mwenendo mwema, bila kujali kupigiwa makofi au

lawama, na wanapaswa kushikamana na haki kwa sababu ya manufaa yake. {1T 458.4}

"Wanawake wanapaswa kufunika viungo vyao vya mbali na moyo (miguu na mikono- limbs) kwa kuzingatia afya na faraja (comfort). Miguu na mikono yao vinahitaji kuvikwa ili vipate joto kama ilivyo kwa wanaume. Urefu wa mavazi ya mtindo haukubaliki kwa sababu kadhaa: {1T 459.1}

"1. Ni ufujaji na pia sio lazima kuwa na vazi lenye urefu kiasi cha kufagia barabara na mitaa. {1T 459.2}

"2. Vazi ambalo urefu wake hukusanya umande kutoka kwenye nyasi, na matope kutoka mitaani, na kwa hivyo ni siyo safi. {1T 459.

“3. Katika hali yake ya uchafu na kutokaa vizuri, vazi hili hukokota uchafu na kukutana na vifundo vya miguu (ankles) ambavyo havijalindwa vya kutosha, na inavipa baridi kwa haraka na hivyo kuhatarisha afya na maisha. Hii ni moja wapo ya sababu kubwa za ugonjwa wa uvimbe kwenye njia za hewa kama

pua na kifua kikuu (Catarrh na Scrofulus) . {1T 459.4 }

"4. Urefu usio wa lazima huleta uzito wa ziada kwenye makalio na mfumo wa uyeyushaji wa chakula. {1T 459.5} ""

3. Huzuia kutembea, na pia mara nyingi huzuia njia kwa watu wengine. {1T 459.6}

"Bado kuna mtindo mwingine wa mavazi ambao unaigwa na tabaka la wale wanaoitwa wanamatengenezo wa mavazi. Wanaiga mfano wa jinsia nyingine kadri iwezekanavyo (wana. Wanavaa kofia, suruali, fulana, kanzu, na buti, sehemu ya mwisho ambayo ni ndiyo angalau ina busara kupita zote katika mtindo wa vazi hili. Wale wanaovaa na kutetea mtindo huu wa mavazi hubeba kile kinachoitwa matengenezo ya mavazi kwa njia ya kutopendeza na kupitiliza. Kuchanganyikiwa kutakuwa matokeo. Wengine wanaopokea vazi hili wanaweza kuwa sahihi katika maoni yao kwa ujumla juu ya swala la afya, lakini wangekuwa na jukumu kubwa katika kufanikisha mazuri zaidi ikiwa hawatajihusisha sana na suala la mavazi kwa kupitiliza kiasi hicho. {1T 459.7}

"Kwa mtindo huu wa mavazi, Agizo la Mungu limegeuzwa na maelekezo Yake maalum hayajazingatiwa. Kumbukumbu la Torati 22:5: "Mwanamke asivae mavazi yampasayo mwamume, wala mwanamume asivae mavazi ya mwanamke; kwa maana kila afanyaye mambo hayo ni machukizo kwa Bwana Mungu wako." Mungu asingependa watu Wake wachukue mtindo huu wa mavazi. Sio mavazi ya adabu, na hayafai kabisa kwa wanawake waadilifu na wanyenyekevu, ambao wanadai kuwa wafuasi

wa Kristo. Makatazo ya Mungu hayazingatiwi sana na wote wanaotetea kuondoa tofauti ya mavazi kati ya wanaume na wanawake. Msimamo uliokithiri, au uliopitiliza, uliochukuliwa na baadhi ya wanamatengenezo wa mavazi juu ya somo hili unadhoofisha mvuto wao. {1T 459.8}

"Mungu aliweka tofauti ya wazi kati ya mavazi ya wanaume na wanawake, na amezingatia umuhimu kiasi cha kutosha, hata kutoa maelekeo wazi juu yake; kwani mavazi yale yale yatakapovaliwa na jinsia zote mbili yatasababisha mkanganyiko na ongezeko kubwa la uasi. Mtume Paulo angekuwa hai, na kuwaona wanawake wanaodai utauwa kwa mtindo huu wa mavazi, angekemea. 'Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujistiri, pamoja na adabu nzuri na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu, au lulu, wala kwa nguo za thamani; bali (kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri ucha Mungu). Umati wa wale wanaojiita Wakristo hupuuza kabisa mafundisho ya mitume, na huvaa dhahabu, lulu, na mavazi ya gharama kubwa. {1T 460.1}

"Watu waaminifu wa Mungu ni nuru ya ulimwengu na chumvi ya dunia, na wanapaswa kukumbuka daima kuwa mvuto wao ni wa thamani. Ikiwa wangebadilisha mavazi marefu sana kwa yale mafupi yaliyokithiri, wangeweza, kwa kiwango kikubwa, kuharibu mvuto wao. Wasioamini, ambao ni jukumu lao kunufaika na kutafuta kuwaleta kwa Mwana-Kondoo wa Mungu, watachukizwa. Maboresho mengi yanaweza kufanywa katika mavazi ya wanawake kwa kuzingatia afya bila kufanya mabadiliko makubwa kuchukiza mtazamaji. {1T 460.2}

"Mwili haupaswi kubanwa hata kidogo na mavazi ya ndani ya kubana ambayo yanatengenezwa na mifupa ya nyangumi

(corsets- Wanawake huvaa hizi, hata leo, kubana tumbo ili kiuno kionekane kidogo-google picha). Mavazi yanapaswa kuwa katika mtindo unaoruhusu mapafu na moyo kufanya kazi kwa urahisi. Vazi linapaswa kufika chini kidogo ya buti, lakini pia linapaswa kuwa fupi vya kutosha kutosafisha uchafu wa barabara bila kuinuliwa na

mkono. Nguo fupi kidogo kuliko hivi itakuwa sahihi, inayofaa, na yenye afya kwa wanawake wakati wa kufanya kazi zao za nyumbani, na haswa kwa wale ambao wanalazimika kufanya kazi za nje. (lakini iwe chini ya magoti kwa kukaa na kusimama). Kwa mtindo huu wa mavazi, sketi moja nyepesi, au mbili zaidi, ndio zaweza hitajika, na hii inapaswa kuwekwa vifungo mpaka kiunoni au kuzuiwa kwa kamba. Viuno havikuundwa kubeba uzito mkubwa. Sketi nzito zinazovaliwa na baadhi, na kuachwa zikilegea kwenye viuno, zimekuwa sababu ya magonjwa anuwai ambayo hayatibiki kwa urahisi. Wagonjwa hao wanaonekana kutokujua sababu ya mateso yao, na wanaendelea kukiuka sheria kwa kuvifunga viuno vyao na kuvaa sketi nzito, mpaka wanapopata madhara ya ulema wa maisha. Wanapoambiwa makosa yao, wengi huonesha kushangaa, 'Kwanini?, mtindo kama huo wa mavazi ni wa kizamani (zilipendwa!)' Ikiwa ni hivyo inadhuru nini?

Natamani tungekuwa wa ki-zamani katika mambo mengi. Ikiwa tungekuwa na nguvu za zamani zilizowatambulisha wanawake wa zamani wa vizazi vilivyotangulia, ingependeza sana. Sisemi bila kushauri ninaposema kwamba njia ambayo wanawake hujivika,

pamoja na hamu yao ya kula, ndio sababu kubwa ya hali yao dhaifu, ya ugonjwa. Kuna mwanamke mmoja tu kati ya elfu ambaye huvisha miguu na mikono yake kama inavyostahili (hata kichwa nacho ni mbali na moyo na hivyo tunahitaji umakini wakati wa baridi). Kwa urefu wowote wa vazi , miguu na mikono yapaswa

kuvikwa vizuri kama ilivyo kwa wanaume. Hii inaweza kufanywa

kwa kuvaa kitambaa cha ndani tena cha suruali (tunasema laining hata kiswahili-lined pants), ambayo hukusanywa na kuchomekewa kwenye kifundo cha mguu, au kuiachilia na kuwekwa pindo chini; na hii inapaswa kushuka mpaka kwenye kiatu (isigaregare chini).

Miguu, mikono na vifundo vilivyofunikwa hulindwa dhidi ya mkondo wa hewa. Ikiwa miguu na mikono itafunikwa vyema kwa mavazi yenye joto, mzunguko utasawazishwa, na damu itabaki safi na yenye afya kwa sababu haipati baridi au kuzuiliwa katika njia yake ya asili kupitia mfumo. "{1T 460.3}

Utata mkuu ulio katika mawazo ya wengi ni hasa juu ya urefu wa vazi. Wengine wanasisitiza kwamba "juu ya buti," inarejelea sehemu ya juu ya buti zile wavaazo wanaume, ambazo hufika karibu na goti. Endapo ingekuwa kawaida ya wanawake kuvaa buti kama hizo, basi watu hawa hawapaswi kulaumiwa kwa kudai kuelewa hili jambo katika namna hii; lakini kwa kuwa wanawake kwa ujumla hawavai buti kama hizo, watu hawa hawana haki ya kunielewa kama walivyojifanya. {1T 462.1}

Ili kuonesha kile nilichomaanisha, na kwamba hakuna ukinzani

 12

katika shuhuda zangu juu ya mada hii, nitatoa hapa dondoo kutoka kwa hati zangu zilizoandikwa karibu miaka miwili iliyopita: {1T 462.2}

"Tangu nakala kuhusu mavazi ilipoonekana katika Jinsi ya Kuishi (*How To Live*), kumekuwa na mkanganyiko juu ya wazo nililotaka kuwasilisha. Wamekuwa na misimamo mikali ya

kutafsiri juu ya kile nilichoandika kuhusu urefu wa vazi, na kwa kweli walikuwa na wakati mgumu sana juu ya jambo hilo. Kwa maoni yao yaliyopotoka juu ya jambo hilo wamejadili suala la kufupisha mavazi hadi macho yao ya kiroho yamechanganyikiwa kiasi cha kuwaona tu watu kama miti inayotembea.Walifikiri wangeweza kuona ukinzani katika nakala yangu juu ya mavazi, iliyochapishwa hivi karibuni katika Jinsi ya Kuishi "How To Live", na nakala ihusuyo mada hiyo hiyo iliyomo katika *Shuhuda kwa Kanisa*, Nambari 10. Lazima nikiri kwamba mimi ndiye mwamuzi bora wa mambo yaliyowasilishwa kwangu katika maono, na hakuna haja kwa yeyote kuhofu kwamba nitapingana na ushuhuda wangu mwenyewe, au kwamba nitashindwa kugundua mkanganyiko wowote wa kweli katika maoni niliyopewa. {1T 462.3}

"Katika nakala yangu juu ya mavazi katika Jinsi ya Kuishi "How To Live" nilijaribu kuwasilisha mtindo wa mavazi ulio na afya, mzuri, unaokubalika, usio na garama, lakini wenye adabu na ungekuwa mtindo wa mavazi kwa wanawake Wakristo kuvaa, ikiwa wangechagua kufanya hivyo. Labda nilijaribu bila kuelezea bila ukamilifu. Vazi linapaswa kufikia chini kidogo ya buti, lakini

linapaswa kuwa fupi kiasi cha kutosha kuepuka uchafu wa barabarani, bila kuinuliwa kwa mkono.' Baadhi wamedai kwamba juu ya buti, nilimaanisha juu ya buti kama wavaazo wanaume. Lakini kuwa 'juu ya kiatu,' nilikusudia kueleweka kuwa juu ya buti,

 12

au kiatu, kinachovaliwa na wanawake. Laiti ningeliwaza kuwa ningelieleweka vibaya, ningeandika kwa uhakika zaidi. Ingekuwa desturi kwa wanawake kuvaa buti-refu kama wanaume, ningeelewa juu ya udhuru huu vya kutosha kuhusiana na mada hii. Nadhani lugha iliyotumika sasa i wazi, na hakuna haja kwa yeyote kupata mkanganyiko. Tafadhali soma tena: "Vazi linapaswa kufikia chini ya kiatu." Sasa angalia vigezo: 'Lakini linapaswa kuwa fupi kiasi cha kutoburuza chini na kufagia uchafu wa barabara, bila kuinuliwa kwa mkono. Nguo fupi zaidi kuliko hii itakuwa sahihi, inayofaa, na yenye afya kwa wanawake wakati wa kufanya kazi zao za nyumbani, na haswa kwa wale ambao wanalazimika kufanya kazi za nje' {1T 462.4}

"Sioni kama kuna kisingizio kwa mtu mwelewa kupata mkanganyiko na kupotosha maana yangu. Kuhusu urefu wa vazi, kama ningekuwa namaanisha kiatu chenye urefu wa juu kiasi cha kufikia karibu na goti, nilikuwa na haja gani basi ya kuongeza,"Lakini [vazi] linapaswa kuwa fupi kiasi cha kutoburuza chini na kusafisha uchafu wa barabarani, bila kuinuliwa kwa mkono 'Ikiwa buti zenye urefu wa juu ndio zingekuwa zimekusudiwa, nguo hiyo ingekuwa fupi vya kutosha

kujilinda na uchafu wa barabara bila kunyanyuliwa, na lingekuwa fupi kiasi cha kutosha kwa majukumu yote ya ufanyaji kazi. Taarifa zimesambazwa kwamba 'Dada White amevaa mtindo wa vazi la Amerika,' (American costume) na kwamba mtindo huu wa mavazi kwa ujumla unakubaliwa na

huvaliwa na akina dada huko Battle Creek. Nimekumbushwa hapa kwamba 'Uwongo utazunguka ulimwenguni kote wakati Ukweli unaanza kuvaa buti zake.' Dada mmoja aliniambia vikali kwamba alikuwa amepokea wazo kwamba mavazi ya Amerika yangeigwa na akina dada wanaotunza Sabato, na kwamba ikiwa mtindo huo wa mavazi utatekelezwa, asingekubaliana nao, kwani akili yake isingemruhusu kuvaa vazi kama hilo.{1T 463.1}

"Kuhusiana na kuvaa kwangu nguo fupi, ningesema, nina nguo moja tu fupi, ambayo ufupi wake si zaidi ya kimo cha kidole kulinganisha na mavazi nivaayo siku zote. Nimevaa vazi hili fupi mara chache (vazi fupi lilikuwa. Katika msimu wa baridi niliamka mapema, na kuvaa vazi langu fupi, ambalo halikuhitaji kuinuliwa kwa mikono yangu ili kulitoa katika theluji, nilitembea kwa kasi kutoka maili moja hadi mbili kabla ya kifungua kinywa. Nimelivaa mara kadhaa na kwenda ofisini nalo, ninapolazimika kutembea katikati ya theluji nyepesi, au wakati kukiwa na mvua nyingi au matope. Kina dada wanne au watano wa kanisa la Battle Creek wamejiandalia mavazi mafupi ya kuvaa wanapofua nguo na kusafisha nyumba. Gauni fupi halijavaliwa katika mitaa ya jiji la Battle Creek, na halijawahi kuvaliwa katika mkutano.

Maoni yangu yalitumika katika kurekebisha mtindo wa sasa, mavazi marefu yaliyokithiri, yanayoburuza chini, na pia kurekebisha mavazi mafupi sana, yakaribiayo kufika karibu na magoti, ambayo huvaliwa na tabaka fulani. Nilioneshwa kwamba tunapaswa kuachana na msimamo

mkali. Kwa kuvaa mavazi yanayofikia juu ya buti za mwanamke tutaepuka maovu ya mavazi marefu yaliyokithiri, na pia tutaepuka maovu na sifa mbaya ya mavazi mafupi sana. {1T 464.1}

"Ningewashauri wale ambao wanajiandalia vazi fupi kwa madhumuni ya kufanya kazi kuzingatia muonekano na unadhifu katika kuliandaa. Liandae katika utaratibu ulio mzuri, litoshe umbo vizuri. Hata ikiwa ni vazi la kazi, linapaswa kupendeza, na kukatwa kwa mpangilio

Kina dada wanapokuwa katika kazi yao hawapaswi kuvaa mava zi ambayo yatawafanya waonekane kama sanamu za kuwatishia ndege mashambani kama kunguru watoke na wasile mahindi (au nafaka-sanamu za kufukuzia ndege- Scarecrows). Inafurahisha zaidi kwa waume zao na watoto kuwaona wakiwa katika mavazi yanayopendeza, na yanayowakaa vizuri kuliko ilivyo kwa wageni tu kuwaona wanapendeza.

Wake wengine na akina mama hudhani kwamba muonekano wao sio jambo la kuzingatia sana wanapokuwa wanafanya kazi au wanapokuwa mbele ya macho ya waume na watoto zao, lakini wanazingatia sana uvaaji wao mbele ya wale wasio maalum au wa

muhimu sana kwao. Je, heshima na upendo wa mume na watoto si wa kuthaminiwa sana kuliko mgeni na watu wengine? Furaha ya mume na watoto inapaswa kuwa takatifu zaidi kwa kila mke na mama kuliko ile ya watu wengine. Kina dada Wakristo hawapaswi wakati wowote kuvaa mavazi yenye gharama kubwa kupindukia,

lakini wakati wote wanapaswa kuvaa kwa unadhifu, kwa adabu, na afya, kwa kadri kazi yao itakavyowaruhusu. "{1T 464.2}

Mavazi yaliyoelezwa hapo juu tunaamini yanastahili jina la mavazi mafupi ya matengenezo. Yamepitishwa katika Taasisi ya Matengenezo ya Afya ya Magharibi (Western Health Reform Institute, Sanitarium iliyoanzishwa na Ellen White kule Battle Creek 1886) na baadhi ya akina dada huko Battle Creek na maeneo mengine ambayo jambo hilo limeelezwa vizuri kwa watu. Kinyume kabisa na mavazi haya ya adabu ni lile lijulikanalo kama vazi la kimarekani, linalofanana kabisa na mavazi ya wanaume. Linajumuisha v e s t i , suruali, na mavazi yanayofanana na kanzu na kufikia karibu nusu kutoka kwenye makalio hadi goti. Mavazi haya nimeyapinga, kutokana na yale ambayo nimeoneshwa kuwa yanapatana na neno la Mungu; wakati mengine nimeyapendekeza kuwa yenye adabu, yanakaa vizuri mwilini, na rahisi kuchukuliana nayo na yenye afya. {1T 465.1}

Sababu nyingine ambayo ninatoa kama wosia kwa kutilia maanani tena mada ya mavazi ni kwamba kati ya kina dada ishirini waliodai kuamini Shuhuda hakuna hata mmoja


12

aliyechukua hatua ya kufanya matengenezo ya mavazi. Yaweza kusemekana kwamba Dada White kwa ujumla huvaa nguo ndefu zaidi hadharani kuliko mavazi aliyoyapendekeza kwa wengine. Kwa hili najibu, Ninapotembelea mahali pa kuongea na watu ambapo mada hii ni mpya na inafanya watu watofautiane, nadhani

ni bora kuwa mwangalifu na sio kuwafanya watu wazibe masikio yao kwa kuvaa mavazi ambayo yatawapa majaribu ya kufanya wasipendezwe. Lakini baada ya kuleta mada mbele yao na kuelezea msimamo wangu kikamilifu, basi mimi hujitokeza mbele yao katika mavazi ya matengenezo, yanayoonesha mafundisho yangu. {1T 465.2}

Kuhusu suala la kuvaa sketi za hoops, vazi la matengenezo liko mbele yake kabisa. Haliwezi kutumia mtindo huo. Na huu sio muda tena wa kuzungumza juu ya sketi hizo tena, kubwa au ndogo. Msimamo wangu juu ya swali hilo ni vile ilivyowahi kuwa, na natumai kutowajibika kwa kile watu wengine wanachoweza kusema juu ya mada hii, au kwa misingi inayofuatwa na wale wanaovaa gauni hizo. Ninapinga upotovu wa mazungumzo yangu ya faragha juu ya mada hii, na ninaomba kwamba kile nilichoandika na kuchapisha kizingatiwe kama msimamo wangu {1T 465.3}

**Sura ya 13 ya Gombo la nne la Shuhuda — Unyenyekevu katika Mavazi**

Katika Mahubiri Yake ya Mlimani Kristo anawahimiza wafuasi

Wake kutoruhusu akili zao kumezwa na mambo ya kidunia. Anasema waziwazi: "Hamwezi kumtumikia Mungu na mali. Kwa sababu hiyo nawaambieni, Msisumbukie maisha yenu, mle nini au mnywe nini; wala miili yenu mvae nini. Maisha Je! Si zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi? Na mavazi ya nini kuyasumbukia? Fikirini maua ya mashamba, jinsi yameavyo; hayafanyi kazi, wala hayasokoti, nami nawaambia, ya kwamba hata

 12

Sulemani katika fahari yake yote hakuvikwa vizuri kama mojawapo la hayo." [4T 628.1]

Maneno haya yana maana iliyosheheni. Yalikuwa yanatumika katika siku za Kristo, na yanatumika katika siku zetu. Hapa Yesu anatofautisha unyenyekevu wa asili wa maua ya shamba na mapambo ya bandia ya mavazi. Anasema kwamba utukufu wa Sulemani haukuweza kulinganishwa na moja ya maua katika uzuri wa asili. Hapa kuna somo kwa wote wanaotamani kujua na kufanya mapenzi ya Mungu. Yesu amebainisha masumbufu na kutoa umakini kwa mavazi, na ametupa tahadhari, naam, Yeye ameamuru, tusitoe tusiweke umakini mwingi au mawazo juu ya hayo. Ni muhimu tuzingatie kwa umakini Maneno Yake. Sulemani alikuwa amevutiwa sana na mawazo au fikra za maonesho ya nje hata akashindwa kuinua akili yake kwa kuungana kila wakati na Mungu wa hekima. Ukamilifu na uzuri wa tabia vilipuuzwa katika jaribio lake la kupata uzuri wa nje. Aliuza heshima yake na uadilifu wa tabia katika kutafuta kujitukuza mbele ya ulimwengu, na mwishowe akawa dhalimu/dikteta, akidumisha na kuunga mkono ubadhirifu wake kwa kuwaumiza/kuwasaga watu kwa kodi nzito. Kwanza aliharibika moyoni, kisha akamwasi Mungu, na mwishowe akawa mwabudu sanamu. [4T 628.2]

Tunapoona dada zetu wakitoka kwenye usahili wa mavazi, na kukuza upendo kwenye mitindo ya ulimwengu, tunahisi wasiwasi. Kwa kuchukua hatua katika mwelekeo huu wanajitenga na Mungu na wanapuuza mapambo ya utu wa ndani. Hawapaswi kuhisi kuwa

na uhuru wa kutumia muda waliopewa na Mungu katika mapambo yasiyofaa ya mavazi yao. Ni bora kiasi gani kama muda huo ungetumiwa katika kuyachunguza Maandiko, na hivyo kupata maarifa kamili ya unabii na masomo ya uhalisia na kivitendo ya Kristo. [4T 628.3]

Kama Wakristo, hatupaswi kushiriki katika kazi yoyote ambayo hatuwezi kuomba baraka za Bwana kwa dhamiri isiyoshitakiwa. Je! ninyi, dada zangu, katika kazi isiyo ya lazima mnapovaa nguo zenu, mnajisikia kuwa na dhamiri safi? Je! wakati mnapotatanisha akili juu ya mapambo ya mavazi

kama marinda, lesi zilizotariziwa na utepe (ribbon), mnaweza kuinua roho kwa Mungu kwa maombi kwamba azibariki juhudi zenu? Wakati uliotumiwa kwa njia hii unaweza kujitolea kufanya mema kwa wengine na kukuza akili zenu wenyewe. [4T 629.1]

Dada zetu wengi ni watu wenye uwezo mzuri, na ikiwa talanta zao zingetumika kwa utukufu wa Mungu wangefanikiwa kuzileta roho nyingi kwa Kristo. Je! Hawatawajibika kwa roho ambazo wangeweza kuziokoa kama wasingekuwa wabadhirifu wa mavazi na masumbufu ya ulimwengu huu na kudhoofisha nguvu zao walizopewa na Mungu hata kutohisi mzigo wa kazi? Shetani alivumbua fasheni/mitindo ili kuzifanya akili za wanawake ziingizwe sana katika mada ya mavazi ambayo wangeweza kuyafikiria kidogo tu. [4T 629.2]

Wajibu wanaopewa akina mama kulea watoto wao katika malezi na mawaidha ya Bwana hauwezi kutupwa/kuondolewa wakati wanaendelea katika mavazi yao. Hawana wakati wa kuomba au kuchunguza Maandiko ili wapate kuelewa Ukweli na kuwafundisha watoto wao. Siyo upendeleo tu bali ni jukumu la kila mtu kuongezeka kila siku katika kumjua Mungu na Ukweli. Lakini lengo la Shetani linapatikana ikiwa anaweza kubuni kitu chochote ambacho kitavutia akili kwamba hili haliwezi kuwa hivyo. Sababu ambayo watu wengi hawatamani kuhudhuria mkutano wa maombi na kushiriki mazoezi ya kidini ni kwamba akili zao zimejitolea kwa mambo mengine. Wanafanana na ulimwengu katika suala la mavazi; na wakati wanapofanya hivyo, wale ambao wangeweza

 12

kuwasaidia kwa kuruhusu nuru yao iangaze katika matendo mema huimarishwa katika kutokuamini kwao na mwenendo tofauti na watu kama hawa wanaojiita Wakristo. [4T 629.3]

Mungu angefurahi kuona dada zetu wamevaa mavazi safi, rahisi na wakishiriki kwa bidii katika kazi ya Bwana. Wao hawana uhaba wa uwezo, na ikiwa wangetumia vizuri talanta walizonazo, ufanisi wao ungeongezwa sana. Laiti muda wanaoutumia sasa katika kazi isiyo ya lazima wangeutoa katika kutafuta Neno la Mungu na kuwaelezea wengine, akili zao zingetajirishwa

na vito vya Ukweli, na wangeimarishwa na kuongezewa nguvu na juhudi iliyofanywa kuelewa sababu za imani yetu. Laiti Dada zetu wangekuwa Wakristo wa Biblia wenye bidii, wakitafuta kuboresha kila fursa ili kuwaangazia wengine, tungeweza kuona roho nyingi zikikumbatia Ukweli kupitia bidii zao za kujitolea peke yao. Akina dada, katika siku ambayo hesabu za watu zitawekwa sawa-watu watatoa hesabu kutokana na matendo yao, Je, mtahisi raha na faraja kupitia maisha yenu, au mtahisi kuwa uzuri wa mtu wa nje tu ndiyo ulitafutwa, wakati uzuri wa ndani wa roho ulikuwa karibu kupuuziwa kabisa? [4T 629.4]

Je! Dada zetu hawana bidii ya kutosha na ujasiri wa maadili kujiweka bila udhuru kwenye jukwaa la Biblia? (Grounded in the Bible, intergrating Mission and faith-wasimame katika msingi wa Biblia katika utume na maombi). Mtume ametoa maagizo wazi zaidi juu ya jambo hili: "Vivyo hivyo wanawake na wajipambe kwa mavazi ya kujisitiri, pamoja na adabu nzuri, na moyo wa kiasi; si kwa kusuka nywele, wala kwa dhahabu na lulu, wala kwa nguo za thamani; bali kwa matendo mema, kama iwapasavyo wanawake wanaoukiri uchaji wa Mungu." Hapa Bwana, kupitia mtume wake, anasema waziwazi dhidi ya uvaaji wa dhahabu. Hebu wale walio na uzoefu waangalie wasiwapotoshe wengine kwa hatua hii kwa mfano wao. Pete hiyo inayozunguka kidole chako inaweza kuwa sahili/rahisi sana, lakini haina maana, na kuivaa kuna athari mbaya kwa wengine. [4T 630.1]

Hasa wake wa wachungaji wetu wanapaswa kuwa waangalifu

wasiondoke kwenye mafundisho yaliyo wazi ya Biblia juu ya mavazi. Wengi huyatazama maagizo haya kama ya kizamani (old fasheni) sana kuweza kutiliwa maanani; lakini Yeye ambaye aliwapatia wanafunzi Wake haya, alielewa hatari itokanayo na upendo wa mavazi katika wakati wetu na akatutumia barua ya onyo. Je! Tutatii onyo na kuwa wenye busara? Ubadhirifu katika mavazi unaongezeka kila wakati. Mwisho bado. Mtindo unabadilika kila wakati, na dada zetu hufuata kwenye njia yake, bila kujali muda au gharama. Kuna fedha nyingi zinazotumika juu ya mavazi, wakati zinapaswa kurudishwa kwa Mungu anayezitoa. [4T 630.2]

Mavazi sahili/rahisi na safi ya tabaka la maskini mara nyingi huonekana tofauti sana na mavazi ya akina dada matajiri zaidi, na tofauti hii mara nyingi husababisha hisia za masikini kupatwa na aibu (wanaona aibu kwa kuwa na mavazi ya kimasikini). Wengine hujaribu kuiga dada zao ambao ni matajiri zaidi, na hutupa na hurundika na kupunguza mavazi yenye ubora duni ili waweze kuwakaribia wale matajiri kwa mavazi. Wasichana maskini, wakipokea dola mbili kwa wiki kwa kazi yao, watatumia kila senti kuvaa kama watu wengine ambao hawalazimiki kujitafutia riziki. Vijana hawa hawana cha kuweka katika hazina ya Mungu. Na muda wao umechukuliwa sana katika kufanya mavazi yao yawe ya mtindo kama ya dada zao kiasi kwamba hawana muda wa kuboresha akili, kwa kusoma Neno la Mungu, kwa sala ya faragha, au kwa mkutano wa maombi. Akili imebebwa kabisa na pilika pilika za kupangilia jinsi ya kuonekana kama dada zao. Ili kutimiza lengo hili, afya ya mwili, akili, na maadili hutolewa dhabihu. Furaha na upendeleo wa Mungu huwekwa juu ya madhabahu ya mitindo. [4T 631.1]

Wengi hawatahudhuria ibada ya Mungu siku ya Sabato kwa sababu mavazi yao yangeonekana kuwa tofauti na ya dada zao Wakristo kwa mtindo na mapambo. Je! Dada zangu wataweza kweli kutazingatia haya mambo jinsi yalivyo, na Je! Watatambua kabisa uzito wa ushawishi wao kwa wengine? Kwa kutembea katika njia iliyokatazwa kwao, wao binafsi wanawaongoza wengine kwa njia ile ile ya kutotii na kurudi nyuma. Unyenyekevu wa

Kikristo hutolewa kafara kwa maonesho ya nje. Dada zangu, tutabadilishaje haya yote? Je! Tutajiokoa/tutaponaje vipi kutoka kwenye mtego wa Shetani na kuvunja minyororo ambayo imetufunga katika utumwa wa mitindo? Je! Tutapataje fursa zetu zilizopotea? Tutaletaje nguvu zetu katika hatua ya afya, na nguvu? Kuna njia moja tu, nayo ni kuifanya Biblia kuwa kanuni yetu ya maisha. Wote wanapaswa kufanya kazi kwa bidii kuwatendea mema wengine, kukesha kwa maombi, kubeba msalaba uliopuuzwa kwa muda mrefu, na kutii maonyo na maagizo ya Yeye ambaye alisema: "Yeyote atakayenifuata, na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake, anifuate. ” [4T 631.2]

Dada zangu Wakristo, kitazameni kioo, sheria ya Mungu, na muujaribu mwenendo wenu kwa amri nne za kwanza. Hizi hufafanua wazi wajibu wetu kwa Mungu. Yeye Anadai kutoka kwetu mapenzi yasiyogawanyika; na chochote kinachoelekea kufyonza akili na kuibadilisha kutoka kwa Mungu huchukua sura ya sanamu. Mungu wa Kweli, Yule aliye hai amebanwa na kuzongwa-zongwa na mawazo na moyo, na hekalu la roho limetiwa unajisi na ibada ya miungu mingine mbele za Bwana. "Usiwe na miungu mingine ila Mimi," amri inasema. Hebu tuuchunguze moyo, kulinganisha maisha na tabia na sheria na maagizo ya Yehova, halafu tutafute kwa bidii kurekebisha makosa yetu. [4T 632.1]

Amri sita za mwisho zinabainisha majukumu ya mwanadamu kwa watu wenzake. Hapa huletwa kuona majukumu mazito ambayo hukanyagwa kila siku na wale wanaodai kuwa ni watunza amri. Wale ambao wameangazwa na neema ya Mungu, ambao wameasiliwa/wamechukuliwa katika familia ya kifalme, hawapaswi kila wakati kuwa watoto katika kazi ya Bwana. Ikiwa wataboresha kwa busara juu ya neema waliyopewa, uwezo wao utaongezeka na maarifa yao yatapanuka zaidi, na watakabidhiwa nguvu kubwa zaidi za Bwana. Katika kuweka juhudi za zenye ari, zilizoelekezwa vizuri kuwaleta wenzao kuijua Kweli, watakuwa wenye nguvu katika Bwana; na kwa kutenda haki duniani, watapokea thawabu ya uzima wa milele katika ufalme wa mbinguni. Hii ndio fursa ya dada zetu. Na tunapowaona wakitumia muda na pesa za Mungu katika onesho lisilo la lazima la mavazi, lazima tuwaonye kuwa hawavunji

amri nne tu za kwanza, bali pia amri sita za mwisho. Hawamfanyi Mungu kuwa mkuu katika ibada yao, wala hawampendi jirani yao kama nafsi zao. [4T 632.2]

Kristo Ndiye mfano wetu. Lazima tutunze mfano mbele yetu na kutafakari dhabihu isiyo na kipimo ambayo imefanywa kutukomboa kutoka katika dhambi kubwa. Ikiwa tunajikuta tunahukumiwa tunapojitazama kwenye kioo, hebu tusijitokeze zaidi katika uvunjaji wa sheria, bali tuangalie kwenye haki na kusafisha mavazi yetu ya tabia katika damu ya Mwana-Kondoo, ili tusiwe na doa. Hebu tupige kilio kama Daudi: "Fungua

macho yangu, ili nipate kuona maajabu kutoka kwenye sheria Yako." Wale ambao Mungu amewakabidhi wakati na mali wanaweza kuwa baraka kwa wanadamu, lakini ambao wamezifuja vibaya karama hizi bila sababu juu yao na watoto wao, watakuwa na wajibu wa kutisha kukutana kwenye kizingiti cha korti ya Mungu. [4T 632.3]

“Kwa maana, tazama, siku inakuja, ambayo itawaka kama tanuri; na wote wenye kiburi, naam, na wote watendao maovu, watakuwa mabua: na siku inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa majeshi, kwamba haitawaachia mzizi wala tawi. ” Ulimwengu usioamini hivi karibuni utakuwa na kitu cha kufikiria zaidi ya mavazi na muonekano wao; na akili zao zitakaponyofolewa kutoka kwa mambo haya kwa shida na mashaka, watakuwa hawana cha kugeukia. Wao sio wafungwa wa tumaini, na kwa hivyo hawageukie Ngome-Sefarnia 9:12. Mioyo yao itawafelisha kwa uchungu na hofu. Hawajamfanya Mungu kuwa kimbilio lao, na Yeye hatakuwa faraja yao. Atacheka msiba wao na atakejeli wakati hofu yao itakapokuja. [4T 633.1]

Wale walioko miongoni watunza Sabato ambao wamejisalimisha kwa ushawishi wa ulimwengu wanapaswa kupimwa. Hatari za siku za mwisho ziko juu yetu, na jaribio lisilotarajiwa liko mbele ya watu wanaodai kumwamini Mungu. Ukweli wa imani yao utathibitishwa. Wengi wameungana na walimwengu kwa kiburi, ubatili, na kutafuta raha, wakijifariji kwamba wanaweza kufanya hivyo na kuendelea kuwa Wakristo. Lakini ni kujiendekeza kama

huko ndiko ambako huwatenganisha na Mungu na kuwafanya wana wa ulimwengu. Kristo hakutupatia mfano kama huo. Wale tu wanaojikana nafsi zao, na kuishi maisha ya kiasi, unyenyekevu, na utakatifu, ndio wafuasi wa Kweli wa Yesu; na hivyo hawawezi kufurahia jamii ya wapenda ulimwengu. [4T 633.2]

Wengi huvaa kama ulimwengu ili kuwa na kuwavutia au kuwa na ushawishi juu ya wasioamini, lakini hapa wanafanya makosa ya kusikitisha. Ikiwa wangekuwa na ushawishi wa Kweli na wa kuokoa, hebu na waishi sawa na imani yao, waoneshe imani yao kwa matendo yao ya haki, na wafanye tofauti kati ya


12

Mkristo na ulimwengu. Maneno, mavazi, matendo, yanapaswa kuzungumzwa kwa niaba ya Mungu. Ndipo ushawishi mtakatifu utamwagwa juu yao wote wanaowazunguka, na hata wasioamini watatambua kwamba wamekuwa pamoja na Yesu. Ikiwa mtu yeyote anataka kupendezwa na ushawishi wao kwa ile Kweli, hebu waishi sawa na madai ya imani yao na kwa hivyo waige Mfano wa unyenyekevu. [4T 633.3]

Kiburi, ujinga, na upumbavu ni marafiki pacha wa kila wakati. Bwana hukasirishwa na kiburi kinachooneshwa miongoni mwa wale wanaodai kuwa wafuasi Wake. Yeye Anachukizwa na kufuata kwao mitindo isiyofaa, isiyo na afya, isiyo na kiasi, isiyo na adabu au uungwana, na mitindo ya gharama ya kizazi hiki kiovu. (4T 634.1)

Mtindo unatawala ulimwengu; na ulimwengu ni mlezi dhalimu, mara nyingi huwalazimisha watumishi wake kujisalimisha kwenye usumbufu, kukosa faraja na mahangaiko makubwa. Mitindo huleta gharama zisizo na sababu na hukusanya fedha bila huruma. Fasheni, ana nguvu ya kuvutia, na yuko tayari kukosoa na kuwakejeli maskini ikiwa hawatafuata uamsho wake kwa gharama yoyote, hata dhabihu ya maisha yenyewe. Shetani anafurahi kwamba nyenzo zake zinafanikiwa vizuri sana, na kifo huangua kicheko na ujinga unaoharibu afya na bidii yao waabuduo kwenye madhahabu ya Mitindo. (4T 634.2)

Ili kuwalinda watu wa Mungu kutokana na ushawishi mbaya wa ulimwengu, na pia kukuza afya ya mwili na maadili, matengenezo

 12

ya mavazi yaliletwa kati yetu. Haikukusudiwa kuwa nira ya utumwa, bali baraka; sio ili kuongeza kazi, bali kuokoa kazi; sio kuongeza gharama ya mavazi, bali kuokoa gharama. Yangetofautisha watu wa Mungu na ulimwengu, na kwa hivyo kutumika kama kizuio dhidi ya mitindo na uovu wake. Yeye anayejua mwisho tangu mwanzo, ambaye anaelewa asili yetu na mahitaji yetu, - Mkombozi wetu Mwenye huruma, - aliona hatari na shida zetu, na alijishusha kutupatia onyo na maagizo kwa wakati unaofaa kuhusu tabia

zetu za maisha, hata katika chaguzi sahihi za chakula na mavazi. (4T 634.3)

Shetani kila wakati anaunda mtindo mpya wa mavazi ambao utathibitisha kuumiza afya ya mwili na maadili; naye hujiinua akifurahi anapoona wale wanaojiita Wakristo wakikubali kwa shauku mitindo aliyoibuni. Kiasi cha mateso ya mwili kilichokusudiwa na mavazi yasiyo ya asili na yasiyofaa hakiwezi kukadiriwa. Wengi wamekuwa vilema maisha yao yote kwa kufuata kwao matakwa ya mitindo. Maumivu ya mwili na ulemavu, saratani na magonjwa mengine mabaya, ni kati ya maovu yanayotokana na mavazi ya mtindo. (4T 634.4)

Mitindo mingi ya mavazi ambayo haikufaa, na hata yenye kufanya watu waonekane wajinga na kuchekesha imekubaliwa kwa ujumla kwa sababu ilikuwa mtindo/ fasheni inayoendana na wakati. Miongoni mwa mitindo hii hatari kulikuwa na uvaaji wa magauni marefu au sketi refu sana zilizokuwa kama mwamvuli (hoops-angalia picha kwenye google), ambazo mara nyingi husababisha mwonekano usiofaa wa mtu huyo. Kinyume na hili yaliwasilishwa mavazi nadhifu, yenye adabu/kiasi. ya kupendeza, ambayo yangefanya waache yale magauni marefu ya hoops (hups) sana na sketi zilizoburuza ardhi, na kutoa mavazi sahihi kwa miguu na mikono. Lakini matengenezo ya mavazi yalikuwa zaidi ya kufupisha mavazi na kufunika miguu na mikono. Yalijumuisha kila kifungu au kipengele kinachohusu mavazi juu ya mtu huyo. Yaliinua uzito kutoka kwenye viuno kwa kuiweka sketi kutoka kwenye mabega. Yaliondoa gagulo (nguo za ndani) zilizobana, ambazo hukandamiza mapafu, tumbo na viungo vingine vya ndani, na kusababisha kupinda kwa mgongo na m-

Kwa wale ambao mara kwa mara waliyapokea matengenezo ya mavazi, wakithamini faida zake na kuchukua msimamo wao kwa furaha dhidi ya kiburi na mitindo, kwao ilithibitika kuwa baraka. Yalipotengenezwa vizuri, yalikuwa mavazi yanayofaa na thabiti, na yaliwafaa watu wenye akili safi na wakweli, hata kati ya wale wasio wa imani yetu. (4T 635.2)

Swali linaweza kuulizwa: "Kwa nini mavazi haya yamewekwa kando, na kwa sababu gani matengenezo ya mavazi hayatetewi tena?" Sababu ya mabadiliko haya nitasema hapa kwa ufupi. Wakati dada zetu wengi walipokubali matengenezo haya kutoka kwenye kanuni, wengine walipinga mtindo huu rahisi, na mzuri wa mavazi ambao ulitetewa. Ilihitajika shuguli kubwa kuanzisha matengenezo haya miongoni mwa watu wetu. Haikutosha kuwasilisha mbele ya dada zetu faida ya mavazi kama haya na kuwaaminisha kuwa yatapata idhini ya Mungu. Fasheni/Mitindo ilikuwa imewashikilia sana kiasi kwamba kuvunja udhibiti wake lilikuwa zoezi la taratibu sana, katika kutii maagizo ya busara na dhamiri. Na wengi waliodai kukubali matengenezo hawakufanya mabadiliko katika tabia zao mbaya za mavazi, isipokuwa kwa kufupisha nguo na kuifunika miguu na mikono yao. (4T 635.3)

Hii haikuwa yote. Wengine waliopitisha matengenezo hayo hayo hawakuridhika kuonesha kwa mfano binafsi, faida za mavazi, walipoulizwa, sababu zao za kuipokea, na kuacha jambo hilo liwe hivyo. Walitafuta kudhibiti dhamiri za wengine na wao wenyewe.

Ikiwa walivaa vazi hilo, basi wengine lazima waivae. Walisahau kuwa hakuna aliyelazimishwa kuvaa mavazi ya matengenezo. (4T 636.1)

Halikuwa jukumu langu kusisitiza mada juu ya dada zangu. Baada ya kuiwasilisha mbele yao kama nilivyooneshwa, niliachia dhamiri zao kufanya utendaji. Hatua za urekebishaji zinaendana kila wakati na dhabihu. Zinadai kwamba upendo wa raha, masilahi ya ubinafsi, na tamaa ya kujiinua zifanyike chini

ya kanuni za haki. Yeyote aliye na ujasiri wa kurekebisha lazima atakutana na vizuizi. Atapingwa na uharibifu wa wale ambao biashara au raha yao huwafanya wawasiliane na wauzaji wa mitindo, na ambao watapoteza watu kwa sababu ya mabadiliko. (4T 636.2)

Hisia nyingi mbaya ziliundwa na wale ambao walikuwa wakisihi kila wakati, mavazi ya matengenezo juu ya dada zao. Na kwa wale wenye msimamo mkali, matengenezo haya yalionekana kuwa ndiyo jumla ya dhehebu la dini yao. Ilikuwa ni mada ya mazungumzo na mzigo wa mioyo yao; na hivyo akili zao zuligeuzwa kutoka kwa Mungu na ile Kweli. Walishindwa kutunza roho ya Kristo na kudhihirisha ukosefu mkubwa wa adabu ya kweli. Badala ya kuthamini mavazi kwa faida yake halisi, walionekana kujivunia tu wimbi la haya matengenezo ya mavazi. Labda hakuna mada ambayo imewahi kutokea kati yetu ambalo imesababisha ukuzaji wa tabia bainishi, kama somo hili la matengenezo ya mavazi. (4T 636.3)

Wakati vijana wengi wakipokea mavazi haya, wengine walijitahidi kuachana na msalaba kwa kujiingiza kwenye mapambo mengine ya ziada, na hivyo kuyafanya matengenezo haya kuwa laana badala ya baraka. Kuhusu wale ambao waliyachukulia matengenezo ya mavazi kwa kusita maishani mwao, kutokana na hali ya wajibu, kwao ikawa nira nzito. Wengine, ambao kwa dhamiri walikuwa wanamatengenezo wenye bidii zaidi, walidhihirisha ukosefu wa utulivu, mpangilio na unadhifu katika mavazi yao. Matengenezo

haya hayakufanywa kulingana na muundo ulioidhinishwa. Wengine walikuwa na aina za suti-magauni ya kitambaa kimoja, pochi kingine na suruali kingine. Wengine wakavaa sketi refu sana, kiasi kwamba nchi moja tu ya suruali ndiyo ilionekana, na hivyo kulifanya gauni liwe na uwiano mbaya na lisilo na ladha nzuri. Mavazi haya ya kutisha na machafu (yanaburuza mitaa) yalichukiza wengi ambao wangefurahishwa na mavazi sahihi ya matengenezo. (4T 636.4)

Wengine walisumbuka sana kwa sababu sikufanya mavazi kuwa jambo la jaribio la imani, na wengine kwa sababu niliwashauri wale ambao walikuwa na waume wasioamini au watoto, kwamba wasiyakumbatie mavazi ya matengenezo,

 12

kwani yanaweza kusababisha kutokuwa na furaha kitu ambacho kingeweza kupinga mema yote yanayopatikana kutokana na matumizi yake. Kwa miaka nilibeba mzigo wa kazi hii na kazi ya kuanzisha msawaziko/usawa wa mavazi miongoni mwa dada zetu. (4T 637.1)

Katika maono niliyopewa huko Battle Creek, Januari 3, 1875, nilioneshwa hali ya mambo ambayo nimeiwasilisha hapa, na kwamba utofauti kadhaa wa mavazi ulikuwa ni jeraha kwa kusudi la Ukweli. Kile ambacho kingethibitisha baraka, ikiwa kilipitishwa kwa usawa na imevaliwa vizuri, ilifanywa kuwa aibu, na, wakati mwingine, hata fedheha. 4T 637.2

Wengine ambao walikuwa wamevaa mavazi hayo waliugua juu yake kama mzigo mzito. Lugha ya mioyo yao ilikuwa: "Hebu kiwe chochote isipokuwa hiki. Ikiwa tulijisikia huru kuachana na mtindo huu wa kipekee, kwa hiari tungekubali mavazi rahisi/manyenyekevu, yasiyokatwa, ya urefu wa kawaida. Miguu na mikono vingeweza kufunikwa vizuri kama hapo awali, na tunaweza kupata faida zote za afya ya mwili, kwa juhudi ndogo. Inahitajika kazi kubwa ili wengi wakumbatie mavazi ya matengenezo kwa njia inayofaa." Manung'uniko na malalamiko yalikuwa yakiharibu utauwa muhimu sana. (4T 637.3)

Sikuwa na mzigo wa Shuhuda juu ya mada ya mavazi. Sikuitaja kwa njia yoyote, ama kuitetea au kuilaani. Lilikuwa kusudi la Bwana kudhibitisha kwa watu Wake wanaodai kumwamini na kufunua nia za mioyo yao. Kwenye mikutano ya makambi mara

 12

chache sana nilikuwa na chochote cha kusema juu ya mada hii. Niliepuka maswali yote na sikujibu barua yoyote. (4T 637.4)

Mwaka mmoja uliopita mada ya mavazi njozi iliwasilishwa tena mbele yangu. Niliona kwamba dada zetu walikuwa wakiondoka kwenye usahili wa injili. Watu wale wale ambao walikuwa wamehisi kwamba mavazi ya matengenezo ni muhimu, na ambao walidai kwamba kuwa hawatashawishiwa na roho ya ulimwengu, sasa walikuwa wamekumbatia mitindo waliyowahi kuilaani hapo

awali. Nguo zao zilipambwa na mapambo yote yasiyo ya lazima ya ulimwengu kwa njia isiyostahili kwa Wakristo na tofauti kabisa na imani yetu. (4T 637.5)

Kwa hiyo kumekuzwa kiburi cha moyo kilichoendekezwa na watu wanaodai kuwa wametoka ulimwenguni na kuwa tofauti. Uvuvio wa Maandiko unatangaza kwamba urafiki wa ulimwengu ni uadui na Mungu; lakini watu Wake wametumia wakati wao na mali waliyopewa na Mungu juu ya madhabahu ya mitindo. (4T 638.1)

Watu wetu wamekuwa wakijipanga upya katika kazi ya matengenezo. Hekima, maamuzi na hukumu vimeonekana kupooza. Ubinafsi na upendo wa kujionesha umekuwa ukiharibu moyo na kuzorotesha tabia. Kuna tabia inayokua ya kutoa dhabihu afya na upendeleo wa Mungu juu ya madhabahu ya mtindo unaobadilika kila wakati, usioridhisha kamwe. (4T 638.2)

Hakuna mtindo wa mavazi unaofaa zaidi kuvaliwa kwenye vituo vya tiba kuliko mavazi ya mategenezo. Wazo linalofurahiwa na wengine, kwamba vazi hilo lingeondoa hadhi au faida/maslahi ya taasisi hiyo, ni kosa. Ni mavazi hayo tu ambayo mtu angetarajia kuyapata hapo, na yasingepaswa kudondoshwa. Katika mavazi haya wasaidizi wangeweza kufanya kazi zao kwa juhudi kidogo kuliko inavyohitajika sasa. Nguo kama hiyo ingehubiri mahubiri yake yenyewe kwa wateja wa mitindo. Tofauti kati ya mavazi yao yasiyofaa, yasiyo na mpangilio, na yaliyotuna, basi yangefuatiwa na mavazi ya matengenezo, yaliyowakilishwa vyema, yanayopendeza kwa kuwa rahisi na yenye usahili katika kutumiwa

na viungo vya mwili, na yangekuwa na mazingira yenye kufundisha zaidi. Wagonjwa wengi wangefanya uboreshaji mkubwa ikiwa wangekubali mabadiliko ya mavazi. (4T 638.3)

Tunasikitika kwamba ushawishi wowote ulipaswa kuletwa dhidi ya mavazi haya safi, na nadhifu ya kawaida, yenye afya. Moyo wa asili husihi kila wakati kupendelea desturi za ulimwengu, na ushawishi wowote huelezea

kwa nguvu mara kumi wakati ukitumiwa katika mwelekeo mbaya. (4T 638.4)

Wakati hakuna aliyelazimishwa kuvaa mavazi ya matengenezo, watu wetu wangeweza na wangethamini maslahai/faida zake na kuyakubali kama baraka. Matokeo mabaya ya njia tofauti inaweza sasa kuonekana. Katika kituo cha tiba/Sanitarium, matabibu na wasaidizi wameyaacha sana maagizo ya Bwana juu ya mavazi. Usahili sasa ni nadra. Badala ya mavazi safi, yasiyopambwa, ambayo kalamu ya Uvuvio imeyaagiza, karibu kila mtindo wa mavazi unaweza kuonekana. Hapa, kama mahali pengine, wale wale ambao walilalamikia kazi inayohitajika kuandaa mavazi ya matengenezo sasa wamepitiliza sana kwa kujipamba bila ulazima. Yote haya huhusisha muda mwingi na kazi nyingi kiasi kwamba wengi wanalazimika kutumia muda wa kazi yao maradufu, zaidi kabisa ya ile ambayo ingewagharimu ikiwa mavazi yangetengenezwa kwa urahisi/usahili kama inavyokuwa kwa wanawake wanaodai kuwa na utauwa. Utengenezaji wa nguo hizi za mtindo unaoongoza, mara nyingi hugharimu zaidi kuliko kitambaa chenyewe. Gharama ya malighafi au nyenzo huwa maradufu mara nyingi kwa mapambo madogo tu. Hapa kiburi na ubatili huoneshwa, na ukosefu mkubwa wa kanuni ya ile Kweli huonekana. Ikiwa watatosheka na mavazi mepesi na rahisi, wengi ambao wanategemea kujikimu kimaisha kwa mapato yao ya kila wiki tu, wangeweza kujishonea wenyewe. Lakini hili sasa haliwezekani, na gharama ya fundi-nguo huchukua kiasi kikubwa

kutoka kwenye mishahara yao midogo. (4T 639.1)

Mungu alikusudia mavazi ya matengenezo kuwa kama kizuizi cha kuzuia mioyo ya dada zetu kutengwa na Yeye Mwenyewe kwa kufuata mitindo ya ulimwengu. Wale ambao walikiondoa kizuizi hicho hawakubeba mzigo wa kukwepa hatari ambazo lazima ziwafuate. Wengine walio katika nafasi za uwajibikaji wamekuwa na ushawishi katika kupendelea mila za kiulimwengu na kinyume kabisa na kiwango cha Biblia. Wamefanya sehemu yao katika kuleta hali ya sasa ya ulimwengu na kurudi nyuma. (4T 639.2)

Mungu amekuwa akiwajaribu watu Wake. Aliruhusu ukimya wa Shuhuda kuhusu mavazi, ili dada zetu waweze kufuata mwelekeo wao na hivyo kukuza kiburi halisi kilichopo mioyoni mwao. Ilikuwa kwa ajili ya kujiwekea kizuzi na kujikana nafsi na hali ya sasa ya ulimwengu ndiyo sababu mavazi ya matengenezo yalipendekezwa. Wengi walifyonza wazo hilo kwamba mavazi haya yalikuwa ya lazima ili kuwahifadhi kutoka katika kufuata mitindo; lakini Bwana amewaruhusu wathibitishe kuwa kiburi kilithaminiwa katika mioyo yao, na kwamba hivi ndivyo tu wangeweza kufanya. Sasa imeoneshwa kuwa walihitaji kizuio/kizuizi cha matengenezo ya mavazi. (4T 639.3)

Ikiwa dada zetu wote wangevaa mavazi mepesi, yasiyopambwa ya urefu wa wastani, mavazi haya yangempendeza Mungu zaidi, na yangekuwa na ushawishi mkubwa zaidi ulimwenguni, kuliko utofauti uliowasilishwa miaka minne iliyopita. Kwa kuwa dada zetu kwa ujumla hawakukubali mavazi ya matengenezo kama yanavyopaswa kuvaliwa, mtindo mwingine, tofauti sasa umewasilishwa. Vitambaa vya mavazi havipaswi kuwa na mambo mengi na michoro, bali viwe rahisi tu bila rangi nyingi. Uangalifu huo huo unapaswa kutolewa kwenye mavazi ya kufika miguuni na mavazi mafupi. (4T 640.1)

Je! Dada zangu watakubali mtindo huu wa mavazi na kukataa kuiga mitindo ambayo imepangwa na Shetani na kubadilika kila wakati? Hakuna mtu anayeweza kusema ni mtindo gani wa kituko utakaofuata. Watu wa dunia ambao huduma yao moja tu ni hii,

 12

"Tutakula nini, na tutavaa nini?" hawapaswi kuwa kigezo chetu. (4T 640.2)

Wengine wamesema: "Baada ya kuvaa mavazi haya, nitafanya mambo kuwa wazi zaidi." Sasa, ikiwa kulingana na mitindo ya ulimwengu ni sawa na inampendeza Mungu, liko wapi basi hitaji la kufanya mabadiliko? Lakini ikiwa ni makosa, Je, ni bora kuendelea na makosa kwa muda mrefu zaidi kuliko inavyopaswa kufanya mabadiliko? Hapa hapa tungewakumbusha bidii na juhudi, ustadi na uvumilivu, uliodhihirishwa katika kuandaa mavazi yenu kulingana na mitindo. Je! Isingekuwa sifa ya kuonesha bidii sawa sawa kuifanya ifanane

na kiwango cha Biblia? Muda wa thamani na mali zilizotolewa na Mungu zilitumika kutengeneza mavazi hayo; na sasa uko tayari kutoa dhabihu ya nini ili kurekebisha mfano mbaya ambao umekuwa ukiutoa kwa wengine? (4T 640.3)

Ni aibu kwa dada zetu kusahau tabia zao takatifu na wajibu wao kwa Mungu kiasi cha kuiga mitindo ya ulimwengu. Hakuna udhuru kwetu isipokuwa upotovu wa mioyo yetu wenyewe. Hatutoi ushawishi wetu kwa njia kama hiyo. Haiendani kabisa na madai yetu ya imani ambayo hutufanya tuwe mabaradhuli machoni pa walimwengu. (4T 641.1)

Nafsi nyingi ambazo zilikuwa na hakika na ile Kweli, zimeongozwa kuamua dhidi ya Ukweli kwa sababu ya kiburi na upendo wa ulimwengu uliooneshwa na dada zetu. Mafundisho yaliyohubiriwa yalionekana wazi na yenye usawa, na wasikiaji walihisi kwamba msalaba mzito lazima uinuliwe na wao katika kubeba Ukweli. Wakati watu hawa walipoona dada zetu wakifanya maonesho mengi katika mavazi, walisema: "Watu hawa huvaa kama sisi kabisa. Hawawezi kuamini kile wanachokiri; na, baada ya yote, lazima wadanganyike. Endapo kweli wangelidhani kwamba Kristo angekuja hivi karibuni, na kesi ya kila nafsi ingeamuliwa kwa uzima wa milele au kifo, wasingeweza kutumia wakati na pesa kuvaa kulingana na mitindo iliyopo." Akina dada hao wanaojiamini kuwa waumini hawakujua sana kama mavazi yao yalikuwa mahubiri! (4T 641.2)

Maneno yetu, matendo yetu, na mavazi yetu ya kila siku ni

wahubiri wanaoishi, wanaokusanya pamoja na Kristo au kutawanya mbali. Hili sio jambo dogo linalopaswa kupitishwa na mzaha. Somo la mavazi linahitaji tafakari nzito na sala nyingi. Watu wengi wasioamini wamehisi kuwa hawakuwa wakifanya vema katika kujiruhusu wenyewe kuwa watumwa wa mitindo; lakini wanapoona wengine wanaodai kuiamini Kweli kwa hali ya juu ya utauwa wakifurahi kuvaa kama watu wa ulimwengu wanavyovaa, wakifurahia upuuzi, wanaona kuwa hakuna kosa katika jambo kama hilo. (4T 641.3)

"Sisi," alisema mtume huyo Paulo aliyevuviwa, "tumefanywa tamasha kwa ulimwengu, na kwa malaika, na kwa wanadamu." Mbingu yote inaandika ushawishi wa kila siku ambao wanaodai kuwa wafuasi wa Kristo huushinikiza juu ya ulimwengu. Dada zangu, mavazi yenu yanamwakilisha Kristo na Ukweli mtakatifu au ulimwengu. Je, ninyi mnamwakilisha nani? Kumbukeni lazima sote tujibu kwa Mungu kwa ushawishi tunaouunda kwa watu. (4T 641.4)

Tusingeweza kwa njia yoyote kuhimiza uzembe katika mavazi. Hebu mavazi yafae na yawe mazuri. Ingawa ni nguo ya senti kumi tu (kaniki au calico), inapaswa kuwekwa kwa unadhifu na usafi. Ikiwa hakuna manung'uniko, mvaaji hawezi kuokoa kitu kwa kukifanya mwenyewe, lakini anaweza kuokoa jumla kidogo kwa kuosha na kupiga pasi nguo hiyo mwenyewe. Familia hujifunga mzigo mzito kwa kuwavika watoto wao kulingana na mitindo. Ni kupoteza muda kiasi kikubwa. Ni ujinga sana kuosha na kupiga pasi mavazi ya mtindo huu bila kuonekana kuwa huo ni mzigo. (4T 641.5)

Je! Ni kwa nini dada zetu wamnyang'anye Mungu huduma inayomfaa, na kumnyang'anya hazina Yake ya pesa ambayo wangeitoa kwa ajili ya kusudi Lake, badala yake wanatumikia mitindo ya ulimwengu huu? Mawazo ya kwanza na bora hutolewa kwa ajili ya mavazi; muda unapotea na pesa zinapotea. Utamaduni wa akili na moyo umepuuzwa. Tabia inachukuliwa kuwa ya umuhimu mdogo kuliko mavazi. Pambo la roho la upole na utulivu lina

thamani isiyo na kikomo, na ni upumbavu wa kutisha kabisa kupoteza fursa na mengineyo katika harakati hizi za kipuuzi/kijinga ili tu kushugulika na mapambo haya ya roho. (4T 642.1)

Akina dada, tunaweza kufanya kazi nzuri kwa Mungu ikiwa tutataka. Mwanamke hajui nguvu zake. Mungu hakukusudia kwamba uwezo wake wote uingizwe katika kuuliza: Nile nini? Ninywe nini? na Nivae nini? Kunalo kusudi kubwa kwa mwanamke, naam, hatima kubwa. Mwanamke anapaswa kukuza na kupalilia nguvu zake, kwani Mungu anaweza kuzitumia katika kazi kubwa ya kuokoa roho kutoka katika uharibifu wa milele. (4T 642.2)

 12

Siku ya Jumapili makanisa maarufu huonekana kama ukumbi wa maonyesho, michezo au filamu (theatre) kuliko mahali pa kumwabudu Mungu. Kila mtindo wa mavazi huoneshwa hapo. Masikini hawana ujasiri wa kuingia katika nyumba hizo za ibada. Maneno yafuatayo yalisikika katika masikio yangu kutoka kwa mchungaji katika moja ya makanisa hayo ya mitindo: "Kanisa linatoa nafasi nzuri sana ya kusoma na kujifunza mitindo hiyo. Ninaweza kuona athari za mitindo tofauti ya mavazi; na, Je, mnajua, ninapata faida kubwa katika shughuli zangu kwa kutazama athari za mavazi mbalimbali kwenye muundo na rangi tofauti. Je! Mliona hicho kiatu kikubwa na kofia hiyo nzuri? Najua jinsi vilivyotengenezwa. Nimekuwa nikichukua masomo siku nzima hapo, ambayo nitayatumia kwa vitendo. " (4T 642.3)

Hakuna neno hata moja lililosemwa juu ya Kristo au juu ya mahubiri yaliyohubiriwa hapo. Nami nikawaza moyo ni kwa jinsi gani ndivyo Yesu anavyoliona kundi hilo, na maonesho yao ya mapambo na mavazi ya kupindukia? Ni aibu gani ambayo nyumba ya Mungu inavyooneshwa kwa watu! Je! Kristo angekuwa duniani, na angepaswa kuyatembelea makanisa kama hayo, si asingewafukuza wale walioidhalilisha nyumba ya Baba Yake? (4T 643.1)

Lakini ubaya mkubwa ni ushawishi kwa watoto na vijana. Mara tu watoto wanapokuja ulimwenguni, huwa wanakabiliwa na mielekeo ya mitindo. Watoto wadogo husikia zaidi juu ya mavazi kuliko wokovu wao. Wanaona mama zao wakitafuta kwa bidii mambo au

vitu vya mitindo kuliko Biblia. Ziara nyingi hufanywa kwa muuzaji wa bidhaa na wauza kofia za kike kuliko kanisani. Maonesho ya nje ya mavazi hufanywa kwa matokeo makubwa kuliko mapambo ya tabia. Magombezo/makaripio makali hutolewa kwa yule ambaye amechafua mavazi mazuri, na akili inakuwa na sikitiko na kukasirishwa kwaajili ya kukanywa na kuwekewa kizuizi cha kila wakati. (4T 643.2)

Tabia mbaya haimfadhaishi mama kama mavazi machafu. Mtoto hutega sikio zaidi juu ya mavazi kuliko utu wema, kwani mama anajua zaidi mitindo kuliko anavyomjua Mwokozi wake. Mfano wake mara nyingi

huwazungushia vijana mazingira yenye sumu. Adui, aliyejificha katika vazi la mitindo, anajiingiza ndani ya watoto. (4T 643.3)

Usahili wa mavazi utamfanya mwanamke mwenye busara aonekane ni mwenye ufanisi au faida bora. Tunahukumu tabia ya mtu kwa mtindo wa mavazi yaliyovaliwa. Nguo sahili huonekana kusaliti ubatili na udhaifu. Mwanamke mwenye kiasi, mcha Mungu atavaa kwa heshima. Hamu iliyosafishwa, akili iliyokuzwa, itafunuliwa katika uchaguzi wa mavazi rahisi na yanayofaa. (4T 643.4)

Kuna pambo ambalo halitaangamia kamwe, ambalo litakuza furaha ya wote wanaotuzunguka katika maisha haya, na kung'aa kwa mng'ao usiofifia katika siku zijazo za milele. Ni mapambo ya roho ya upole na kujishusha. Mungu ametualika kuvaa mavazi tajiri ya kiroho. Kwa kila kujitazama ndani ya kioo, waabudu mitindo wanapaswa kukumbushwa juu ya roho iliyopuuzwa. Kila saa iliyotumiwa chooni/bafuni katika kujiangalia na jinsi utakavyopendeza inapaswa kukemea dhamiri zao kwa kuiacha akili kutumiwa kwa njia ya upotevu/uharibifu. Ndipo kunaweza kuwepo na matengenezo ambayo yangeinua na kukuza malengo na madhumuni yote ya maisha. Badala ya kutafuta mapambo ya dhahabu kwa nje, juhudi ya ari yapaswa kufanyika ili kupata hekima hiyo ambayo ina thamani kubwa kuliko dhahabu safi, ndio, ambayo ni ya thamani zaidi kuliko yakuti. (4T 643.5)

Wale wanaoabudu katika madhabahu ya mitindo wana nguvu kidogo ya tabia na nguvu kidogo ya mwili. Wanaishi bila kusudi kubwa, na maisha yao hayatimizi mwisho mzuri. Tunakutana kila

mahali na wanawake ambao akili na mioyo yao yote imeingizwa katika upendo wao wa mavazi na maonesho. Nafsi ya mwanamke imepunguzwa na kuhafifishwa, na mawazo yake yamejikita katika hali yake duni, na ya kudharauliwa. Msichana aliyevaa vizuri alikuwa akiwapita wanaume kadhaa barabarani alipokuwa anatembea na mmoja wao alimuulizia akitaka kujua habari zake kama yeye ni binti wa namna gani. Jibu lilikuwa hili: "Yeye hufanya pambo nzuri katika nyumba ya baba yake, lakini vinginevyo hana faida." Inasikitisha kwamba wale wanaodai kuwa

wanafunzi wa Kristo wanapaswa kudhani ni jambo zuri kuiga mavazi na adabu ya mapambo haya yasiyofaa. (4T 644.1)

Petro anatoa maagizo ya maana juu ya mavazi ya wanawake Wakristo: "Kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele, na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi, bali kuwe utu wa moyoni usioonekana,
katika mapambo yasiyoharibika, yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za Mungu. Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu na kuwatii waume zao." Tunachohimiza ni kufuata maagizo ya Neno la Mungu. Je! Sisi ni wasomaji wa Biblia na wafuasi wa mafundisho ya Biblia? Je! Tumtii Mungu, au tufuate mila za ulimwengu? Tutamtumikia Mungu au mali? Je! Tunaweza kutarajia kufurahia amani ya akili na kibali cha Mungu wakati tunatembea kinyume kabisa na mafundisho ya Neno Lake? (4T 644.2)

Mtume Paulo anawasihi Wakristo wasifanane na ulimwengu, bali wabadilishwe kwa kufanywa upya nia zao, "ili mpate kujua mapenzi ya Mungu yaliyo mema, na ya kukubalika, na ukamilifu." Lakini wengi wanaodai kuwa watoto wa Mungu hawahisi hatia yoyote dhidi ya kufuata desturi za ulimwengu katika uvaaji wa dhahabu na lulu na mlolongo wa yale ya gharama kubwa. Wale ambao ni waangalifu sana katika kuvaa vitu hivi huchukuliwa kama wenye mawazo finyu, washirikina, na hata washabiki. Lakini ni Mungu ndiye anayejishusha ili kutupa maagizo haya; hayo ni matamko ya Hekima Isiyo na Ukomo, na wale wanaoyapuuza haya,

 12

hufanya hivyo kwa hatari na hasara yao wenyewe. Wale wanaoshikamana na mapambo yaliyokatazwa katika Neno la Mungu wanathamini kiburi na ubatili moyoni. Wanatamani kuwavutia watu. Mavazi yao yanasema:

Niangalieni; nimependeza. Kwa hivyo ubatili uliomo katika asili ya mwanadamu unazidi kuongezeka kwa kujitosheleza. Akili inapowekwa kwenye kumpendeza Mungu peke yake, mapambo yote ya mtu hayatakiwi. (4T 644.3)

Mtume anaweka mapambo ya nje kinyume kabisa na roho ya upole na utulivu kisha anashuhudia juu ya thamani kwa kulinganisha na hiyo ya pili: "Mbele za Mungu ana thamani kubwa." Kuna utofauti wa wazi kati ya upendo wa mapambo ya nje na neema ya upole, roho tulivu. Ni wakati tu tunapotafuta katika mambo yote kuendana na mapenzi ya Mungu ndipo amani na furaha vinapotawala nafsini. (4T 645.1)

Upendo wa mavazi huhatarisha maadili na kumfanya mwanamke kuwa kinyume cha mwanamke Mkristo anayejulikana na upole na kiasi. Mavazi ya kujivunia, ya kupindukia mara nyingi huhimiza tamaa katika moyo wa mvaaji na huamsha tamaa moyoni mwa mtazamaji. Mungu huona kuwa uharibifu wa tabia mara nyingi hutanguliwa na kuendekezwa kwa kiburi na ubatili katika mavazi. Anaona kwamba mavazi ya gharama hukaba koo la shauku ya kufanya mema. (4T 645.2)

Kadri watu wanavyotumia mali zaidi katika mavazi, ndivyo watakavyokuwa na uwezo mdogo wa kuwalisha wenye njaa na kuwavika walio uchi; na mito ya neema, ambayo inapaswa kuwa inapita kila wakati, inakauka. Kila dola iliyookolewa kwa kujikana dhidi ya mapambo yasiyokuwa na maana inaweza kutolewa kwa wahitaji au inaweza kuwekwa katika hazina ya Bwana ili kudumisha injili, kuwatuma wamishenari katika maeneno ya mbali, kuongeza machapisho yabebayo miale ya nuru kwa roho katika giza la makosa. Kila dola inayotumiwa inamnyima mtumiaji fursa ya kufanya mema. (4T 645.3)

Dada yangu, umetumia muda gani kwa vitu visivyohitajika, wakati ambao ulipaswa kutoa hesabu kwa Mungu? Ni pesa kiasi gani zilizotumiwa kufurahisha mapenzi yako ya kufikirika na kupata pongezi za mioyo iliyo batili tu kama ulivyo mwenyewe? Hizo zilikuwa pesa za Mungu. Je! Ni mema gani unaweza kuwa umeyafanyia na hizo pesa! Na Je, umepata hasara gani katika maisha haya, na katika siku zijazo, maisha ya kutokufa, kwa kutofanya hivi! Kila roho itahukumiwa kulingana na matendo yaliyofanywa mwilini. Mungu anasoma madhumuni na nia. Kila kazi na kila jambo la siri liko wazi kwa Yule anayeona yote. Hakuna mawazo, neno, au kitendo asichokiona. Yeye Anajua kama tunampenda

na kumtukuza Yeye au tunajiinua wenyewe. Yeye Anajua kama tunaweka mapenzi yetu juu ya mambo ya juu, ambapo Kristo ameketi mkono wa kuume wa Mungu, au juu ya mambo ya kidunia, ya mwili na ya kishetani. (4T 646.1)

Unapoweka nguo isiyo na maana/manufaa juu ya mwili wako, unazuia kuvisha walio uchi. Unaposambaza katika meza zako 'kwa kuchafua meza' kwa chakula cha gharama kubwa, unapuuza kuwalisha wenye njaa. Rekodi yako, Wewe unayedai kuwa Mkristo ikoje? Tafadhali nakusihi, usijiingize kwenye utapanyaji wa kuumiza na wa kipumbavu ambao Mungu anautaka katika hazina Yake, na sehemu ambayo wanapaswa kupewa maskini. Hebu Tusijivike mavazi ya gharama, bali, kama wanawake wanaokiri kuwa na utauwa, tuwe na matendo mema. Hebu kilio cha mjane na yatima kisipande mbinguni dhidi yetu. Wala damu ya roho isipatikane kwenye mavazi yetu. Wala wakati wa thamani wa majaribio upositezwe kwa kuenzi fahari ya moyo. Je! Hakuna masikini wa kutembelewa? hakuna wenye macho hafifu unaoweza kuwasomea Neno la Mungu? Hakuna waliokata tamaa, waliopoteza imani ambao wanahitaji maneno yako ya faraja na maombi yako? (4T 646.2)

Kadri Mungu alivyokufanikisha, Je! Utoshelevu wa kiburi na ubatili vimekuwa vikiongezeka kwa kasi? Wakati ukitumia muda mzuri kwa kujifunza kuhusu mavazi, mapambo ya ndani hayazingatiwi; hakuna ukuaji wa neema. Badala ya kuwa na mawazo ya kimbingu zaidi, unazidi kuwa na nia ya kidunia. Tamaa

za upumbavu na zenye kuumiza, uchu wa chakula, hupunguza hisia zako kuelekea vitu vitakatifu. Kwa nini kila mtu anayedai kumpenda Yesu asiukimbie huu uendekezaji mbaya unaoharibu roho? Ulimwengu una wazimu mbele ya onesho na mitindo na anasa. Uzembe ni thabiti na unazidi kuongezeka kwa hofu kuu. Kwa nini Wakristo wasiwe wakweli kuhusu madai yao ya juu, ya imani! (4T 646.3)

Kristo anaaibishwa na wale wanaojiita kuwa wafuasi Wake. Je! Ni kwa jinsi gani tunafanana naye? Je! Mavazi yetu yanapatana na mahitaji ya Biblia? Sitaki dhambi za watu ziwe juu yangu, na nitapiga tarumbeta kwa sauti

 12

kubwa. Kwa miaka mingi nimekuwa na ushuhuda ulio wazi na nimeamua juu ya mada hii, kwa machapisho na kwa sauti ya juu. Sikuepuka kutangaza shauri zima la Mungu. Lazima niwe huru na kuhusika na damu ya watu wote. Ukweli kwamba ulimwengu na kiburi hubeba karibu ulimwengu wote kwenye gari lake sio kisingizio kwa Mkristo mmoja kufanya kama wengine. Mungu amesema: "Usiwafuate wengi kufanya maovu." (4T 647.1)

Dada zangu, msichezee/msizidharau roho zenu na Mungu. Nimeoneshwa kuwa sababu kuu ya kurudi nyuma kwenu ni upendo wenu wa mavazi. Hii inasababisha kupuuzwa kwa majukumu makubwa, na mnajikuta mkiwa na uhaba wa upendo wa Mungu mioyoni mwenu. Bila kuchelewa, kataeni sababu ya kurudi nyuma kwenu, kwa sababu ni dhambi dhidi ya nafsi zenu wenyewe na dhidi ya Mungu. Msifanywe wagumu kwa sababu ya udanganyifu wa dhambi. Mtindo unadhoofisha akili na kuitafuna hali ya kiroho ya watu wetu. Utii wa mitindo umeenea katika makanisa yetu ya Waadventista wa Sabato na unafanya zaidi ya nguvu nyingine yoyote kuwatenganisha watu wetu na Mungu. Nimeoneshwa kuwa sheria za kanisa letu zina mapungufu sana. Maonesho yote ya kiburi katika mavazi, ambayo ni marufuku katika Neno la Mungu, yanapaswa kuwa sababu tosha ya nidhamu kwa kanisa. Ikiwa kuna mwendelezo, licha ya maonyo na kusihi na maombi, na bado kuna kuyafuata mapenzi yaliyopotoka, hilo linaweza kuzingatiwa kama uthibitisho kwamba moyo haujafungamanishwa na Kristo. Ubinafsi, na ubinafsi tu, ndio kitu cha kuabudiwa, na mmoja wa

wale wanaojiita Wakristo atawaongoza wengi mbali na Mungu. (4T 647.2)

Kuna dhambi mbaya juu yetu sisi watu wa imani, kwamba tumewaruhusu washirika wetu wa kanisa kuvaa kwa njia isiyoendana na imani yao. Lazima tuamke mara moja na tufunge mlango dhidi ya vivutio vya mitindo. Tusipofanya hivyo, makanisa yetu yataharibika. (4T 648.1)


12

## KIJUZUU CHA MAVAZI MATENGENEZO

## YA MAVAZI

**Wito kwa Watu kwa Niaba Yake BWANA**

Sisi sio waabudu mizimu (spiritualists). Sisi ni wanawake Wakristo, tunaoamini yote ambayo Maandiko yanasema kuhusu kuumbwa kwa mwanadamu, anguko lake, mateso na huzuni zake na ole zake kwa sababu ya kuendelea na uasi, juu ya tumaini lake la ukombozi kupitia Kristo, na wajibu wake wa kumtukuza Mungu katika mwili na roho yake ili kuokolewa. Hatuvai mtindo wa mavazi hapa unaowakilishwa vazi lisilokuwa la kawaida (odd), ili tuweze tu kuvutia macho ya watu wengine. Hatuna tofauti zaidi ya mtindo wa kawaida, na hatuna chochote cha ajabu au kisicho cha kawaida (odd). Tunachagua kukubaliana na wengine kwa nadharia na kwa vitendo, ikiwa tunaweza kufanya hivyo, na wakati huo huo kupatana na sheria ya Mungu, na sheria za utu wetu. Tunaamini kuwa ni makosa kutofautiana na wengine, isipokuwa ni lazima kutofautiana ili kutenda lile lililo sawa (right). Katika kubeba msalaba wa kupitisha vazi la matengenezo, tunaongozwa na hisia ya wajibu. Na ingawa inaweza kuonekana kuwa ni jambo la kuchukiza kwa wale wanaoongozwa na mitindo, tunadai kwamba ndiyo mtindo wa mavazi unaofaa zaidi, wenye kiasi na kujistahi, na wenye afya zaidi unaovaliwa na mwanamke. {PH134 1.1}

Tumeihesabu gharama ya kuonekana tofauti machoni pa wale wanaohisi kulazimishwa kupigia magoti fasheni/mtindo. Na tunaamua kwamba mwishowe italipa kujaribu kufanya lile lililo sawa au haki, ingawa kwa sasa tunaweza kuonekana isivyo kawaida machoni pa wale ambao watajitoa mhanga kwaajili ya maisha yaliyo rahisi, yenye faraja, na afya, kwenye madhabahu ya mtindo. {PH134 2.1}

Pia tumeangalia ukweli kwamba mwenendo wetu katika suala hili la mavazi utawasababishia marafiki zetu hisia za kutopenda, na tumezingatia yale mambo ambayo yalisisimua hisia zao kwa chuki dhidi ya vazi la matengenezo. Tunapokuwa miongoni mwa watu baki, tunapaswa kuwa kama wale waumini wa mizimu", kutokana na ukweli kwamba baadhi ya tabaka hilo hufuata kile kinachojulikana kwa kawaida kama "vazi fupi." Na swali linaulizwa mara kwa mara, "Je, ninyi ni wanamizimu?" Kwa kujibu swali hili, na kumpa msomaji baadhi ya sababu zinazotufanya tuchukue vazi lisilo na mtindo (Vazi lenye staili isiyo kwenye fasheni inayoendelea), ndiyo maana kijuzuu hichi kidogo kimetolewa sasa. Tunafahamu vyema kwamba baadhi ya wale walioiunga mkono imani ya umizimu (spiritualists), juu ya thamani yao ya kimaadili ambayo kivuli cha kutokuwa na uhakika kimetupwa, na ubadhirifu na uasherati miongoni mwao, wamechukua mavazi mafupi (inchi nane au tisa kutoka kwenye ardhi), na kwamba bidii yao katika kufanya hivyo. Chini ya mazingira ya kipekee, yaweza kuwachukiza watu dhidi ya kitu chochote cha aina hiyo. (watu wenye imani potofu ya mizmu, walikuwa wakivaa kwa adabu, wengine wakaona, ili kuonekana wao hawafanani nao, basi wavae nguo fupi, na kupinga eti kwasababu kundi lile wana Mafundisho potofu) {PH134 2.2}

Inawezaje kuwa vinginevyo? Watu wamefungwa na mitindo. Hawaelewi faida za staili yetu ya mavazi. Na ni jambo la kuchukiza zaidi kwao kwani linafanana, katika baadhi ya mambo, na lile linalovaliwa na baadhi ya washiriki wa umizimu wenye dini

yenye kutiliwa shaka. Kwa hakika tunawakaribisha wanawake wa dini ya umizimu kwa moyo wote, kupata faida na baraka ya manufaa yote ya mavazi yanayofaa, yenye afya, na (yenye urefu ufaao, nadhifu. yanakaa vizuri mwilini na kutengenezwa ipasavyo,) mavazi yenye kiasi au kujistahi kwa kweli, na kutamani yangekuwa thabiti na haki katika mambo mengine. {PH134 3.1}

Katika hali iliyopo, watu wanaweza kuona kupitishwa kwa mtindo wetu wa mavazi kuwa hatua ya ujasiri kwa upande wetu, inayoonyesha sisi tu huru


12

zaidi kuliko vile tulivyo na ladha nzuri ya mavazi. Nao wanaweza kutulaumu. Wanaweza kushughulika nasi kwa futuhi na kejeli kwa kurejelea mavazi yetu. Wanaweza hata kutoa hotuba za uchungu kwa sababu ya mwenendo wetu katika jambo hili. Lakini kazi yetu itakuwa, kwa neema ya Mungu, kufanya kazi kwa subira kurekebisha makosa yao, kuondoa chuki au ubaguzi wao, na kuweka mbele yao sababu za kwa nini tunapinga mitindo maarufu na inayopendwa ya mavazi ya wanawake; pia kwa baadhi, sababu ya kwa nini sisi tumeipitisha kuwa yetu. Tunapinga mtindo maarufu au wa mavazi ya mwanamke (au ule unaopendwa na wengi), {PH134 3.2}

1. Kwa sababu haufai kwa kukosesha watu raha, au urahisi katika kufanya kazi za nyumbani, katika kupanda juu na chini wakati mikono yote miwili imeshikilia vitu, mkono wa tatu unahitajika kushikilia sketi ndefu. Mwangalie mdada huyo akipita kuelekea kwenye chumba chake akiwa na mtoto mikononi mwake, na mikono yake yote miwili ikiwa imejaa vitu, na akikanyaga sketi yake ndefu, naye hujikwaa anapojongea mbele. Anajua mtindo maarufu na unaopendwa ni bughuda na hatari- yaani haufai. Lakini kwasababu ni fasheni/ mtindo, basi ni lazima uvumiliwe, naye aendelee tu kujikaza kwa kuvaa. {PH134 4.1}

Ikiwa ataenda kwenye bustani yake kutembea au kufanya kazi kwenye maua yake, ili kujipatia hewa ya asubuhi yenye kuburudisha pasipo kuinua sketi yake kwa mikono miwili, sketi yake itaburuzwa naye atavutwa huo kwenye uchafu na umande,

mpaka gauni lake lilowe na matope. Mtindo unaongoza maisha yake, nguo yake katika kesi hii, hakika hutumiwa kama aina ya dekio la barabara. Hii inamfanya asumbuke sana. Lakini kwa ajili ya fasheni au mtindo ni lazima avumilie na kujikaza kisabuni tu. {PH134 4.2}

Katika kutembea barabarani, mashambani, kijijini, au katika jiji lenye watu wengi, sketi yake ndefu hufagia uchafu na matope, na kudeki mate ya ugoro (tumbaku), na kila aina ya uchafu. Wanaume wengine wakati mwingine masikini jamani, hukanyaga nguo hizi ndefu kwa bahati mbaya, wakati wanawake wanapita na kuzichana/kuzitatua. Hili ni jaribu, na wakati


12

mwingine hukera; na sio rahisi kila wakati kukarabati na kusafisha nguo hizi zilizochafuliwa na zilizochanika. Lakini wanaendana kwa mapatano na fasheni/mtindo, na haya yote lazima yavumiliwe. {PH134 4.3}

Katika usafiri wa magari, katika viti vya treni, na mabasi, nguo za mtindo huu, hasa zile ambazo zina sketi za mwamvuli wa hoops na zenye kuburuza ardhi, wakati mwingine sio tu zinawazuia wale wavaaji kujongeza mwili, bali na wengine pia njiani au kwenye familia wanapata shida; nasi tunafikiri kwa huruma kwamba, laiti nguvu inayotawala mitindo isingekuwepo, na hatua zingechukuliwa kuwaondolea usumbufu. {PH134 5.1}

Tunapinga mtindo maarufu wa mavazi ya mwanamke yanayopendwa, {PH134 5.2}

2. Kwa sababu mtindo huu hauna afya. Kwani unabana kiuno vibaya sana, hata mtu anaweza kujiua kwaajili ya kutopumua vizuri kama vile maumbile ya binadamu yanavyopaswa (asili), na kusababisha tabia ya kupumua tu kutoka juu ya mapafu; na kutozingatia katika kutoweka uzito wote usio wa lazima kwenye makalio, na sketi zingine za ndani (za mifupa) na urefu uliopitiliza, hapa kuna mengi ambayo yanaweza kusemwa kuhusiana na kuharibu afya kwa mtindo wa mavazi ya mwanamke; lakini tunapendekeza kwa wakati huu tu yafuatayo: {PH134 5.3}

(a) Hulemea na kuzuia matumizi huru ya miguu. Hii ni kinyume na mpango wa Mungu katika kumpatia mwanamke kutenda kazi

zake na pia kujipatia afya. {PH134 5.4}

(b) Humfungia ndani mara kwa nyingi wakati afya yake inamtaka afurahie mazoezi katika hewa safi na yenye kuchangamsha ya mbinguni. Akitoka nje kwenye theluji nyepesi, baada ya manyunyu ya mvua au au kwenye umande wa asubuhi au jioni, yeye hulowesha sketi yake na tope na hata mvua, hufanya vifundo vya miguu visivyolindwa vipate baridi. Ili kuzuia hili, anaweza kubaki akiwa amejifungia ndani ya nyumba, na kuwa

mlegevu na mnyonge sana hivi kwamba anapolazimika kutoka nje ana uhakika wa kupata mafua, kikohozi, (korona), kifua kikuu, na hata kifo.
{PH134 5.5}

Inaweza kusemwa kwamba anaweza kungojea jua liwake ili afanye matembezi yake kwani unyevunyevu utakuwa umekwisha na hivyo kutojipatia maji kwenye nguo yake yenye mshono unaofanya iburuzike. Shida ni kwamba akitoka baadaye anaweza kuhisi maumivu ya joto au jua kali la kiangazi cha mchana. Ndege huenda pamoja na nyimbo zao za kumsifu Muumba wao, na wanyama wa porini hufurahia pamoja nao ule uchangamfu wa asubuhi; na joto la jua linaposhuka, viumbe hawa wa asili na wenye afya hurudi kwenye kivuli. Lakini huu ndio wakati wa huyu mwanamke wa vazi refu linaloburuza chini, kuondoka na mavazi yake ya fasheni/mtindo! Ndege wanapotoka kwenda kufurahia hewa ya asubuhi yenye kutia nguvu, yeye ananyimwa fadhila hii tajiri ya Mbinguni. Wanapotafuta kivuli cha baridi na kupumzika, yeye ndiyo anatokezea na kwenda kuteseka kutokana na joto, uchovu, na unyonge. {PH134 6.1}

(c) Vazi hili linamwondolea ulinzi huo dhidi ya ubaridi na unyevunyevu unaofanya sehemu za chini ya miguu kupata shida ya mfumo wa afya. Ili kufurahia hali nzuri ya afya, lazima kuwe na mzunguko sahihi wa damu. Na ili kupata mzunguko mzuri wa afya, maisha ya mwanadamu lazima yawe na mzunguko mzuri wa damu, sehemu zote za mwili lazima ziwe na mkondo mzuri wa mtiririko

wa damu. Mtindo huvisha kifua cha mwanamke huyu kwa nguo tele, na wakati wa msimu wa baridi hupakia magunia, koti, shela na manyoya kifuani, hadi hawezi kuhisi baridi, isipokuwa mikono na miguu yake imevikwa, ambayo sasa ina ukosefu wa kufunikwa na nguo zinazofaa, na kisha huwa na ubaridi, na kuungua kwa baridi. Moyo unafanya kazi ya kusukuma damu hadi kwenye miguu na mikono yake isiyofunikwa vizuri, lakini damu inayorudishwa kutoka huko inakuwa ya baridi, kwa kukosa kuvishwa vizuri kwa viungo hivi (miguu na mikono). Na ule wingi wa nguo juu ya kifua, ambacho ndicho gurudumu kubwa la maisha, huingiza damu

nyingi kwenye mapafu na ubongo, na kutoa msongamano wa damu.{PH134 6.2}

Mikono na miguu ina mishipa mikubwa, ili kupokea kiasi kikubwa cha damu, ambayo joto, lishe, kunyumbulika, na nguvu, vinaweza kutolewa kwao. Lakini wakati damu imepozwa kutoka kwenye miguu na mikono, mishipa yao ya damu husinyaa, jambo ambalo linafanya kiasi cha mzunguko muhimu cha damu ndani yake kuwa mgumu zaidi. Mzunguko mzuri wa damu huhifadhi damu safi, na hulinda afya. Mzunguko mbaya wa damu huacha damu kuwa najisi/chafu, na husababisha msongamano kwenye ubongo na mapafu, na kusababisha magonjwa ya kichwa, moyo, ini na mapafu. Staili ya mtindo wa mavazi ya mwanamke ni mojawapo ya sababu kuu za magonjwa haya yote ya kutisha. {PH134 7.1}

Lakini uovu hauishii hapa. Akina mama hawa wa mitindo husambaza magonjwa yao kwa watoto wao dhaifu. Na huwavisha wasichana wao wadogo na wanyonge kwa njia isiyofaa kama wanavyojivika wenyewe, na hivi punde wanawaleta nao kwenye hali ya ulemavu, au, ya mateso makubwa kuliko ya mfu aliye kaburini. Hivyo mtindo hujaza makaburi yetu mengi na majeneza mafupi-fupi au madogo madogo ya watoto hawa, na hujaza nyumba kwa watumwa hawa wa mitindo na ubatili. Je, ni lazima hali hii ya mambo ya kusikitisha iendelee? {PH134 7.2}

Tunapinga staili za mitindo ya mavazi ya mwanamke, {PH134 8.1}

3. Kwa sababu, chini ya hali fulani, tukisema kwa uchache, sio

kujistahi vyema zaidi, kwa sababu inafanya umbo la kike lionekane au kutokezea zaidi. Kisha uovu huu unazidishwa sana na kuvaa sketi za hoops. Wanawake walio na nguo ndefu, haswa ikiwa wameongezea gagulo za hoops (za chuma au mifupa ili kufanya ile sketi itue na kuwa kama mwavuli), hawa wanapopanda na kushuka ngazi, na wanapopita kwenye mlango mwembamba wa treni au basi la abiria, au wanaponyanyua sketi zao, h ufagia matope barabarani.

wakati mwingine hufichua umbo lao kwa kiwango ambacho chaweza kumfanya mtu anayejistahi vyema kupata aibu/soni usoni. {PH134 8.2}

Baada ya kuona baadhi ya makosa ya mtindo maarufu wa mavazi ya mwanamke, sasa tunataka kuonyesha kwa kurejelea vazi la matengenezo kwamba, {PH134 8.3}

1. Hakuna hoja zinazohitajika ili kuthibitisha kwamba mtindo wetu wa vazi u rahisi zaidi kufanya nao kazi jikoni. Katika kupanda ngazi juu na chini, mikono haihitajiki kushikilia sketi au nguo zetu. Zikiwa na urefu unaofaa, zinajishugulikia zenyewe, huku mikono yetu ikiwa inatumika vyema zaidi. {PH134 8.4}

Tunaweza kwenda nje kwenye theluji mpya isiyokanyagwa, au baada ya mvua kunyesha, na, ikiwa mikono na miguu yetu imefunikiwa vyema kabisa, mwili wote ni mkavu na ulio katika hali sawa. Hatuna hofu ya kupata ugonjwa wa mafua au kikohozi tunaposafiri, hatulemewi na sketi tunazozikanyaga kwa bahati mbaya katika matembezi yetu ya asubuhi. Katika majira ya kuchipua au ya joto, tunaweza kutembea na kufanya kazi katika maua yetu bila kuwa na hofu ya kuumia kwenye umande wa asubuhi na mapema. Na kisha, sehemu za chini za sketi zetu, ambazo hazijatumiwa kama dekio, zinakuwa kavu, safi, na zinazotupa starehe kwa vile huondoa usumbufu, na hazitulazimishi kuziosha na kuzisafisha, jambo ambalo sio rahisi kila wakati kulifanya, wakati mambo mengine muhimu yanahitaji wakati na umakini wetu.

{PH134 9.1}

Katika kuingia na kutoka kwenye magari ya farasi, katika kuangalia maboksi, masanduku, na samani/fanicha nyingine chakavu, na katika kutembea juu ya vinjia vya miguu vilivyochakaa au vyenye mashimo, ambapo misumari imeinuka inchi moja au mbili juu kwenye mbao za madaraja, nguo zetu hazikutwi na chngamoto au matatizo, kama kuraruliwa/kuchanwa. Kwetu sisi, hili ni suala linalofanya maisha kuwa rahisi. {PH134 9.2}

Mikono, kichwa na miguu yetu inalindwa ipasavyo kutokana na ubaridi na unyevunyevu, ili kuhakikisha mzunguko wa damu unakuwa sawa, pamoja na baraka zake zote. Tunaweza kuchukua mazoezi katika hewa ya wazi, katika umande wa asubuhi au jioni, au baada ya dhoruba inayoanguka ya theluji au mvua, bila hofu ya kupata magonjwa ya kupumua kama vile kikohozi (cold). Mazoezi ya asubuhi, katika kutembea kwenye hewa huru ya mbinguni, yenye kutia nguvu au kulima maua, matunda madogo, na mboga mboga, ni muhimu kwa mzunguko wa afya ya damu. Ni kinga ya uhakika dhidi ya mafua, kikohozi, msongamano wa ubongo na mapafu, kuvimba kwa ini, figo, mapafu, na magonjwa mengine mia moja. {PH134 10.1}

Ikiwa wanawake hao ambao wanadhoofika kiafya, wanaoteseka kwa sababu ya magonjwa haya, wangevua mavazi yao ya fasheni, wakajivika wenyewe kwa kustarehesha mwili (comfort) na kujipatia mazoezi kama hayo, kwa kuanza mazoezi kwa uangalifu mwanzoni, wao wanaweza kustahimili, na kuongeza kiasi cha mazoezi kwa kadri watakavyoendelea. katika anga ya wazi, kwani inawapa nguvu za kustahimili, na kuachana na madaktari wao na dawa za hospitalini, wengi wao wanaweza kupona kiafya, ili kubariki ulimwengu kwa mfano wao na kazi ya mikono yao. Ikiwa wangewavisha binti zao ipasavyo, wangeweza kuishi ili kufurahia afya, na kuwabariki wengine. {PH134 10.2}

Mama mkristo: Kwa nini usimvishe binti yako kwa starehe/faraja

(comfort) inavyofaa kama vile unavyomvalisha mwanao wa kiume? Katika baridi na dhoruba za majira ya baridi kali, mikono yake na miguu yake huvikwa suruali, kaptura, soksi za sufu, na buti nene. Hivi ndivyo inavyopaswa kuwa; lakini binti yako amevaa kwa kurejelea mtindo wa leo, na sio afya, wala starehe/faraja (comfort). Viatu vyake ni vyepesi, na soksi zake ni nyembamba. Ni kweli, sketi yake ni fupi, lakini viungo vyake vi karibu uchi, vimefunikwa na soksi nyembamba ya flana inayofikia kwenye kaptura yake

ya nylon ambayo ni kama gagulo. Viungo na miguu yake vinapata ubaridi, na huku kakaye ana joto la kutosha mwilini. Viungo vyake vinalindwa na unene wa nguo tatu hadi tano; ila msichana ana kanguo kamoja tu eti kwasababu anavalia mvao wa fasheni ya wasichana uliopo. Je, huoni kwamba yeye ndiye dhaifu? Naye anahitaji utunzaji au umakini wako zaidi. Je, hayuko ndani ya nyumba kwa muda mrefu zaidi, na, kwa hiyo, anakingwa dhidi ya baridi na dhoruba kuliko kakaye? Basi yeye anahitaji huduma maradufu. Lakini akiwa amevalia hivyo kwa kuipendeza fasheni, hakuna kitu cha kutumainia siku zijazo kuhusiana na afya yake isipokuwa miguu baridi kama ilivyo kawaida, ubongo ulioshonana, damu isiyotembea vizuri, maumivu ya kichwa, ugonjwa wa ini na mapafu, na kaburi la mapema.
{PH134 10.3}

Gauni lake linaweza kuwa na urefu wa kutosha; lakini liache lisibane ili atembee kwa uhuru na raha. Kisha ivalishe mikono, kichwa na miguu yake kwa raha/faraja (comfort), kwa busara, na kama vile unavyomfanyia mtoto wako wa kiume; na kisha mwache aende nje na kufurahia mazoezi katika hewa ya wazi, na kuishi akifurahia afya na furaha. {PH134 11.1}

1. Ni kuwa na kiasi, ni kujisetiri. Ndiyo, tunafikiri ni mtindo ambao una kujisetiri na kupendeza, unaovaliwa na mwanamke. Ikiwa msomaji anadhani vinginevyo, Je, anaweza kufungua ukurasa wa picha za zile nguo tena, na kisha achunguze tena taswira inayowakilishwa hapo, na kisha atuambie ni kwa vipi

mtindo huu wa mavazi una kasoro au haufai? Hakika, mshono huo hauendani na fasheni. Ila kuhusiana na hilo, Je, fasheni imetoka wapi? Kumbuka kuwa mitindo haitoki Mbinguni kila wakati, na wala siku zote haitoki kwenye usafi wa moyo, fadhili na wema. {PH134 11.2}

3. Ni kweli kwamba mtindo huu wa mavazi huweka wazi miguu yake ili ionekane. Na ni kwa nini aionee aibu miguu yake iliyofunikwa vizuri, kama vile wanaume wasivyoionea haya miguu yao iliyofunikwa vizuri? Hakuna faida kwake kujaribu kuficha ukweli kwamba anayo miguu. Huu ulikuwa

ukweli uliowekwa muda mrefu kabla ya matumizi ya sketi zinazoburuza ardhi zinazotunishwa na waya au mifupa ya samaki na kuwa kama mwanvuli (sketi za hoops), na kumpa mwonekano kama wa matita ya nyasi kavu za kulisha ng‟ombe (haystack), au gudulia la Uholanzi la kuchekechea siagi (angalia picha mwisho wa kitabu). {PH134 12.1}

Lakini Je, mtindo maarufu wa mavazi ya mwanamke daima huficha miguu yake kutoka kwenye macho ya umma? Hebu mtazame mwanamke huyo akipita kwenye barabara yenye matope, akiwa ameishikilia sketi yake karibu mara mbili mbali na ardhi kuliko kawaida, na kusababisha kufanya miguu yake ya chini iwe wazi wakati wa baridi, na si tu miguu yake ya chini, bali pia sehemu ya miguu ya juu, iko karibu wazi. Mfiduo kama huo wa fasheni hutokea mara kwa mara anapopanda na kushuka ngazi, anaposaidiwa kuingia na kutoka nje ya mabehewa ya treni au mabasi (kwa vile wanamwona hajiwezi, naye anakazania magauni haya tu, ambayo yanafanana kidogo na yale ya vazi la wanawake taifa la Uganda la busuti). Maonyesho haya hayapendezi na hayafanyi maisha kuwa rahisi, na pengine huleta hata aibu; nayo mitindo hii inazidi kuongezeka kila mahali. hakika, inatufanya sisi kuchukua ulazima wa kuwa walinzi wa wema na kiasi/kujisetiri. Lakini siyo sisi ambao tulibuni au kufichua huku kujisetiri feki kunakohusiana na miguu ya mwanamke, lakini tumejaribu tu kutetea mtindo wa vazi ambao tunazingatia kwamba utakuwa msaada na haki, kwa kila njia, ya kujitawala nafsi, kiasi au

kujisetiri kwa kweli. {PH134 12.2}

Je, ni mtindo gani wa mavazi unaoweza kuwa nadhifu zaidi, wenye kiasi na kujisetiri, na kupendeza zaidi kwa wasichana wenye umri wa kuanzia miaka mitano hadi kumi na nne kuliko wa vazi letu tulilopendekeza? Wasimamishe wale wasichana wanaopenda fasheni/mitindo kando ya hawa, na kisha waulizie kuwa, ni mtindo upi haumbughudi mtu (comfortable), ni wa kujisetiri zaidi, na wa kupendeza zaidi. Staili ya mtindo wao sio refu kama wetu; na bado hakuna anayewacheka wale wanaofuata mtindo huo, kwa kuvaa nguo fupi (Inchi 8 au 9 kutoka kwenye unyayo. Viungo vyao vi karibu

uchi/wazi, wakati heshima na afya huvivalisha vyema viungo vya wasichana wengine. Mitindo na kujistahi feki (uwongo) huwatazama wasichana hawa ambao viungo vyao vimevikwa hivi, ili kuleta starehe/faraja (comfort), kiasi, kujistahi na afya, kwa kuogofya, bali hutabasamu kwa wale ambao nguo zao ni fupi sana, na ambao viungo vyao havifurahii, havina adabu au kujisetiri, na vimefunuliwa kwa njia mbaya. Huu ni msalaba na lawama, yaani kwa kutaka kutenda tu haki, mbele ya mdhalimu au mjeuri aitwaye—Mtindo, watu wanajipatia shida nyingi. Hebu Mungu atusaidie kuwa na ujasiri wa kimaadili, wa kutenda haki, na kufanya kazi kwa subira na unyenyekevu katika kazi hii kuu ya matengenezo ya mavazi. {PH134 13.1}

Kwa niaba ya dada zangu waliozingatia vazi la matengenezo,

{PH134 13.2

SOP

Greenville, Montcalm Co., Mich.

## Mapendekezo Machache

1. Tunapendekeza vazi la matengenezo kwa wote. Hatumshurutishi yeyote. Wakati wanawake Wakristo wataona makosa ya fasheni, na faida za vazi letu, na kulivaa kutoka kwa hisia ya wajibu, na kuwa na ujasiri wa kimaadili wa kulivaa popote na kila mahali, basi watajisikia wapo nyumbani kwa furaha na utulivu ndani ya hilo, na kisha wataridhika na kubarikiwa katika

kujaribu kutenda haki. (PH134 13.3)

2. Lakini wale wanaochukua vazi la matengenezo wanapaswa kukumbuka ule ukweli kwamba nguvu ya fasheni ni ya kutisha; na kwamba katika kukutana na huyu bwana mitindo ambaye ni jeuri na katili, wanahitaji hekima, unyenyekevu, na uvumilivu,— na hekima ya kusema na kutenda ili kutowaudhi watumwa wa mitindo isiyo ya lazima; wanahitaji pia

unyenyekevu na subira ya kustahimili watu walioivuta midomo yao kwa kununa semi zao na maneno yasiyopendeza watakayoyatoa. (PH134 14.1)

3. Kwa kuzingatia chuki zilizopo dhidi ya vazi la matengenezo, inakuwa ni wajibu wetu kulikubali ili kuepukana na mambo yote ambayo yanalifanya kuwa la kupingwa isivyo lazima. Vazi hili linapaswa kuwa kama inchi nane au tisa kutoka sakafuni (chini kidogo ya magoti). Sketi haipaswi kutanuka na kuwa kama mwavuli wa hoops. Bali inapaswa kuwa kamilifu kama yale mavazi marefu. Sketi sahihi isiyokuwa nzito, gauni litakaa vizuri na kupendeza kwenye miguu na mikono (PH134 14.2).

4. Sio vazi lolote lililo inchi nane au tisa kutoka sakafuni ndilo la matengenezo. Vazi linapaswa kuwa na mshono unaokubaliwa yaani likatwe katika muundo ulioidhinishwa, na kupimwa kutokana na maelekezo kutoka kwa mtu yule ambaye ana uzoefu katika mtindo huu wa mavazi. (PH134 14.3)

4. Ladha inapaswa kuonyeshwa katika rangi. Usawa katika suala hili, na wale wanaotumia mtindo huu wa vazi, ni muhimu lipendwe na kuwa linalofaa. Rangi izingatiwe. Rangi zilizotulia kama bluu, nk zinaweza kupendekezwa. Wakati rangi zilizofikiriwa zinatumiwa, vile vitambaa vyenye michoro mikubwa au rangi ambazo zinang"aa sana, ambazo zaweza kuonyesha kiburi kwa wale wanaozichagua, zinapaswa kuepukwa. Na ladha nzuri na ya ajabu katika kuzichagua na kuzipanga, rangi tofauti inatakiwa hapo, mfano,

 12

